Nipashe
Alhamisi Januari 24, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579822
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter. ... hetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Mtoto mchanga afa kwa kuliwa na panya


UKURASA 3


ama
ALHAMISI JANUARI 24, 2019
AFYA NA MAZINGIRA
Ukurasa 18
Viungo sita vya mwanadamu vilivyopoteza umuhimu wake
Ukurasa 15
Mwanamume anavyoshikilia tiba kichaa cha mimba
Ukurasa 14
Vijana katika hatari zaidi ya pumu
RC SHINYANGA:
Kila mwaka tunazika darasa na nusu wazazi, shule nzima watoto
Ukurasa 19

UKURASA 13

# Viongozi wa dini walia na kamari

• **Wamwomba** JPM kuingilia kati, wadai inakinzana na kaulimbiu ya ' Hapa Kazi Tu', mwenyewe awajibu na kusema... *Endelea ukurasa 2*



"Vijana wengi sasa wameelekeza nguvu kwenye kamari.
**Zainuddin Adamjee**



"Kuna uhaba wa ajira nchini. Zipo fani ambazo mhitimu hawezi kujiajiri.
**Askofu Cheyo**



"Kujengwe nyumba za ibada maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi kama vile uwanja wa ndege.
**Sheikh Mussa Kundecha**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MMOJA AFARIKI, WATATU WAFUKIWA KIFUSI MGODINI**

MTU mmoja amefariki dunia na wengine watatu kufukiwa na kifusi katika machimbo ya dhahabu ya Nyangalata, Kahama mkoani Shinyanga...

UKURASA WA 26

**MVUA YA DAKIKA 30 YATIKISA MSAFARA WA RC**

MVUA iliyonyesha kwa dakika 30 jana ilisababisha msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nickodemas Mwangela, akiwa na kamati...

## Udasa yaibua mambo mazito

UKURASA 3



## Bosi TIC amvaa Tundu Lissu

UKURASA 3

**MICHEZO** SABABU FIFA KUMFUNGIA WAMBURA MAISHA UK.32
**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais John Magufuli, akizungumza na viongozi wa dini, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.
**PICHA: IKULU**

# Viongozi wa dini walia na kamari

**Na Gwamaka Alipipi**

VIONGOZI wa dini nchini, wamemweleza Rais John Magufuli, mambo 10 wanayopendekeza yafanyiwe kazi katika utawala wake, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kuzuia michezo ya kamari.

Viongozi hao walikutana na Rais Magufuli jana Ikulu jijini Dar es Salaam kwa mazungumzo na kupewa nafasi ya kuzungumzia mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya tano.

Kwenye mazungumzo hayo, viongozi hao walimwelezea Rais magufuli mambo 10 ambayo wanayaona ni changamoto kwa wananchi.

**KAMARI**

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabohora Tanzania, Zainuddin Adamjee, alimweleza Rais Magufuli kuwa, michezo ya kubahatisha imekuwa ikishika kasi nchini bila ya kudhibitiwa.

Alisema vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa, wamekuwa wakijihusisha na kucheza kamari huku vyombo vya habari vikitumika kuhamasisha suala hilo kwa kuweka matangazo ya kampuni za kamari.

"Utakuta mtu anaweka Sh. 10,000, anacheza kamari, halafu akishinda utaona kwenye televisheni anakabidhiwa zawadi yake na Mkuu wa Mkoa au Wilaya," alisema Adamjee.

Kiongozi huyo wa dini alisema nguvu kazi kubwa ya vijana kwa sasa imeelekezwa katika kucheza kamari ili wapate pesa nyingi kwa wakati mmoja.

Wakati wa mkutano uliopita wa Bunge la Bajeti, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alitangaza mapendekezo ya kuongeza kodi kwenye michezo ya kubahatisha inayohusisha ubashiri, mashine, ujumbe mfupi na kasino za mtandao kutoka asilimia 10 hadi 25.

Alibainisha kuwa pendekezo hilo litaiwezesha serikali kupata mapato yanayokadiriwa kufikia Sh. bilioni 26.7 katika mwaka huu wa fedha.

Mwanzoni mwa wiki, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alitangaza kupitia kwa Waziri wa Fedha, David Bahati, kuzuia michezo ya kubahatisha na aina zote za kamari zinazofanyika nchini mwake, kutokana na kuwaathiri wacheza kamari, hususan vijana.

Ilielezwa kuwa michezo ya kamari imekua kwa kasi Uganda katika miaka ya karibuni, huku ikisababisha kuvuruga kipato cha familia kutokana na vijana kutofanya kazi nyingine zaidi ya kushinda kwenye kamari.

Waziri Bahati alisema hakutakuwa na kampuni ya kamari yoyote itakayopewa leseni nchini humo na zilizopo, hazitapewa leseni mpya baada ya zile za awali kumaliza muda wake.

**AJIRA, MAJI, ELIMU**

Askofu wa Kanisa la Moravian Jimbo la Kusini Magharibi, Alinikisa Cheyo, alisema kuna changamoto ya ajira nchini, akieleza kuwa wapo wahitimu ambao fani walizosomea zinawaruhusu kujiajiri bila matatizo yoyote, lakini wapo pia wahitimu ambao fani zao haziwaruhusu kufanya hivyo.

Alisema kuna idadi kubwa ya vijana vijijini ambao wamemaliza elimu ya vyuo vikuu, lakini hawana kazi yoyote ya kufanya.

Askofu Cheyo pia alisema kuna changamoto kubwa ya uhaba wa maji nchini, akibainisha kuwa maeneo mengi, wananchi wanatumia bomba moja kuchota maji.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Amani Lymo, alimweleza Rais Magufuli kuwa, licha ya serikali kuanza kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo, bado kuna changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

"Bado kuna changamoto katika elimu, tunakuomba ikiwezekana uziruhusu kamati za shule pamoja na bodi ziweze kukusanya michango itakayosaidia kuendesha shule," alisema Lymo.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Dodoma, Gervas Nyaisonga, aliyeeleza kuwa sekta ya elimu kuna tatizo.

"Vyuo vilianzishwa kwa sheria na shule zilianzishwa kwa sheria. Kuna vyuo vimezuiwa visidahili wanafunzi, na huyo anayezuia anatumia sheria. Tunategemea ufafanuzi juu ya hili," alisema Nyaisonga.

Mchungaji Lymo pia alimwomba Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kufanya uchunguzi kuangalia namna ya kuwasaidia watu wanaoishi katika hali ya umaskini ili wawe wanapata za afya bila malipo kwa kuwa wakati bima hazikubaliki.

"Nadhani uliona kilichotokea katika Hospitali ya KCMC, tunaomba changamoto kama hizi zitafutiwe ufumbuzi ili kuhakikisha kuwa kile mtu alichokilipia, anakitumia vyema na kunufaika nacho," alisema Lymo.

DEMOKRASIA

Mchungaji Lymo pia alimwomba Rais Magufuli kuruhusu demokrasia nchini, akidai kuwa wananchi wengi wana hofu, hivyo awaachie kidogo wazungumze.

Mwenyekiti wa Kina Mama Waislamu Mkoa wa Dar es Salaam, Pili Abdallah, alimwomba Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kuangalia vizuri namna bora ya kumpangia shule mwanafunzi aliyefaulu.

"Mtoto anayekaa Kata ya Kibada (Kigamboni) anachaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule iliyopo Kata ya Pugu (Ilala), sidhani kama ni sawa," alisema Abdallah.

Sheikh wa Jumuiya na Taasisi ya Kiislamu, Mussa Kundecha, alimwomba Rais Magufuli kuruhusu ujenzi wa misikiti katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi kama vile uwanja wa ndege.

**TAHADHARI UGAIDI**

Katibu Mkuu Ismailia Tanzania, Kasim, alisema shambulio la kigaidi lililotokea nchini Kenya siyo zuri, hivyo kuna haja serikali kuchukua tahadhari.

"Kwa upande wa serikali iangalie hii kitu. Tuna jukumu la kukaa na vijana wetu kama wazazi na viongozi wa dini," alisema Kasim.

Askofu wa Kanisa la Efatha, Josephat Mwingira, alisema miundombinu ya nchi bado ni changamoto kwa kuwa uboreshaji wake kila mwaka umekuwa ukilazimu serikali kubomoa nyumba za wananchi.

Mwingira alipendekeza kuwapo na mfumo mzuri wa miundombinu kwa kuweka wataalamu watakaosimamia ujenzi wa miundombinu nchini.

"Watu wa umeme, barabara, simu, maji wawe na mikakati mizuri na iliyo bora kuhusu ujenzi wa miundombinu, watengeneze mifumo mizuri," alisema.

**MISAMAHA YA KODI**

Askofu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly, David Mwasota, alimwomba Rais Magufuli kuangalia upya hatua ya serikali kufuta misamaha ya kodi kwa taasisi za dini nchini.

Alisema taasisi nyingi za dini zinashindwa kuagiza vitu kutoka nje kwa sababu ya kuwapo kwa kodi katika bidhaa hizo.

**MALIPO YA KOROSHO**

Kiongozi wa Kanisa la Biblia Tanzania, John Mchopa, alisema jambo alilofanya Rais Magufuli kuagiza serikali inunue korosho kutoka kwa wakulima ni zuri, lakini kuna dosari kwenye malipo.

"Uhakiki haufanyiki vizuri. Kuna hata wakulima wa kilo 100 hawajalipwa. Naomba hili jambo la uhakiki liende kwa haraka. Dhamira yako ni njema, lakini kwenye kutenda kuna watu wanapenda kuumiza watu," alisema.

Akijibu hoja ya korosho, Rais Magufuli alisema ameshatoa maagizo kwa mawaziri wanaohusika na kilimo na biashara wahakikishe wakulima wenye kiwango kidogo wanalipwa pesa zao haraka.

"Kamati za uhakiki za korosho washirikiane. Wakague maeneo. Wasaini watu walipwe kutokana na sehemu walipo. Wasikae wanawachelewesha watu kulipwa. Narudia tena... nataka wakulima wa korosho walipwe mapema na fedha zote zipo," alisema.

Kuhusu sekta za elimu na afya, Rais Magufuli alisema kuna taasisi za dini 791 zinazomiliki zahanati 791, vituo 160 hospitali 116, vyuo vikuu 14 na vyuo vikuu vishiriki 12.

Alisema sekta ya elimu ilikuwa imeingiliwa na wajanja ambao walikuwa wanaitumia Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kuwapangia wanafunzi badala ya kuacha wanafunzi wenyewe wachague.

"Pakatokea rushwa mpaka bodi ya chuo kikuu nikaivunja. Chuo cha Udom wanafunzi 7,628 wa kidato cha nne walipelekwa kudahiliwa, wote tuliwafukuza, tukawapeleka wanapostahili kusoma," alisema Rais Magufuli.

Kuhusu misamaha ya kodi kwa taasisi za dini, Rais Magufuli alisema haijafutwa, bali inasimamiwa kisheria.

"Misamaha ya kodi ni sehemu mojawapo watu walikuwa wanatumia kukwepa kodi. Kwa kutambua hilo, serikali ikafuta mianya yote ya kodi," alisema Rais Magufuli.

Alibainisha kuwa mwaka 2016, serikali ilitoa msamaha wa kodi wa Sh. bilioni 19.66 kwa taasisi za dini, mwaka 2017 Sh. bilioni 17.6 na mwaka 2018 Sh. bilioni 47.84.

Kuhusu demokrasia, Rais Magufuli alisema: "Nataka niwahakikishie ndugu zangu, demokrasia ipo. Demokrasia siyo kuruhusu maandamano tu. Demokrasia ina mipaka yake.

"Mmekuwa mkitembea kila mahali, sijui kama mnaona maandamano. Tukifanya hivyo tutashindwa kutawala. Tunataka vyama vyetu viheshimiane kama dini zetu. Narudia tena, hakuna mtu aliyekatazwa kufanya mkutano mahali alipo," alisema Rais Magufuli.

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso (wa pili kushoto), akijadili jambo na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, baada ya kukagua na kupokea taarifa katika chanzo cha maji cha Chole Kwala, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya maji, wilaya ya Kisarawe juzi. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Udasa watishia kuingia mgogoro na serikali

**Na Elizabeth Zaya**

JUMUIYA ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Udasa), imesema watalazimika kuingia katika mgogoro na serikali, ikiwa haitawalipa madai yao ya muda mrefu kufikia mwishoni mwa mwezi huo.

Jumuiya hiyo imedai wanachama wake wanaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 11 kutokana na malimbikizo ya posho ya nyumba ya kuishi na nyongeza ya mishahara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Udasa, Dk. George Kahangwa, alidai wamekuwa wakidai stahiki hizo kwa muda mrefu bila mafanikio.

"Kwa wanataaluma wa UDSM kwa mfano, hadi sasa wanadai kutoka serikalini jumla ya Sh. bilioni 6.272, ikiwa ni deni la kuanzia Januari 2014 hadi Septemba mwaka jana. Pesa nyingine ni Sh. bilioni tano ambazo ni nyongeza ya mishahara iliyotokana na msawazisho wa utaratibu wa utumishi katika vyuo vya umma," alisema Dk. Kahangwa na kuongeza:

"Mwaka jana, Ofisi ya Utumishi wa Umma ilituahidi kwamba serikali ingetulipa madai hayo kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2017/2018, ilipofika Juni ni wana Udasa 102 tu na wengine wachache kutoka vyuo vikuu vingine ndiyo walilipwa, lakini 1,060 waliendelea kusubiri mpaka leo (jana)."

Dk. Kahangwa alisema Udasa pia inadai mishahara ya miezi mitano ya wanataaluma wapya walioajiriwa mwaka 2017 pamoja na nyongeza ya mshahara za kila mwaka na kifuta jasho kwa wastaafu walioko katika mikataba ya kazi na kwamba baadhi ya wastaafu hao wameondoka kazini bila kulipwa hazi zao hizo.

Alisema madai mengine ni baadhi ya wanataaluma

INAENDELEA UK. 8

# Mtoto afa kwa kuliwa na panya

**Na Steven William,** MUHEZA

MTOTO Ibrahim Joseph mwenye umri wa miezi minne, amefariki dunia baada ya kung'atwa na panya mara tatu katika mguu wake wa kushoto akiwa amelala usiku na mama yake mzazi, Veronica Haule.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi katika kitongoji cha Mang'ula kijiji cha Kwabada, Muheza mkoani Tanga.

Diwani wa Kwabada, Fredrick Kazimoto, alisema tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Man'gula na kwamba wakati linatokea, mtoto huyo alikuwa amelala na mama yake mzazi katika kitanda ambacho hakina chandarua ndani ya nyumba yao na usiku huo, lilitokea kundi la panya na kuanza kumshambulia kwa kumla mtoto huyo katikamguu wake huku mama akiwa hana habari kutokana na kulala fofofo.

Kazimoto alisema panya hao wamemla nyama mtoto huyo katika nyayo, kisigino na baadaye kuhamia katika goti kisha kuimaliza ngozi na nyama yote ya mguu na kubakisha mfupa.

Alisema kutokana na panya hao kula mguu wa mtoto huyo, ilisababisha kupoteza maisha usiku huo na baadaye mama wa mtoto huyo alipoamka kutoka usingizini, alikuta mtoto wake amefariki dunia huku mguu wote ukiwa umeliwa na panya na kubaki mfupa.

Akisimulia tukio hilo, Haule alisema ilipofika majira ya saa nne usiku, waliingia kulala kama ilivyo ada kila siku.

INAENDELEA UK. 8

# Bosi TIC ajitosa kumvaa Lissu

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Geofrey Mwambe, amesema atakutana kwa mazungumzo na Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu (Chadema), atakaporejea nchini, ili "kumjengea uelewa zaidi wa masuala ya uwekezaji".

Amesema atafanya hivyo ili asiendelee kufanya kile alichodai upotoshaji wa mambo yanayofanywa na serikali chini ya Rais John Magufuli, kama alivyozungumza kwenye mahojiano ya kipindi cha Hardtalk akiwa Uingereza hivi karibuni.

Mwambe aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua ya Rais Magufuli kuihamisha TIC kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda kuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kumteua Angela Kairuki kuwa Waziri wa Nchi-Uwekezaji.

Mkurugenzi huyo alidai ameshangaa kuona Lissu ameamua kuichafua Tanzania badala ya kuitangaza Tanzania kimataifa licha ya mazuri mengi inayofanya kwa sasa.

Alisema TIC imekuwa na utaratibu wa kuzungumza na viongozi mbalimbali wa sekta na idara mbalimbali za serikali pamoja na wabunge kwa lengo kuwajengea uelewa kwenye masuala yanayohusu uwekezaji.

"Nitafurahi sana nikikutana naye (Lissu), nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Manyoni na yeye ni Mbunge wa Singida Mashariki, tulikuwa tumepakana wakati mwingine nilikuwa nakaimu nafasi ya Mkuu wa Wilaya kule kwake, kuna kipindi nilikuwa namtafuta tukae jimboni kwake," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza: "Nilitamani nikutane naye tangu siku nyingi kuzungumzia masuala ya maendeleo, nitakutana naye tu kwa sababu ni watu ambao tunawasiliana, nitakutana naye ili kuhimizana inapotokea masuala ya nchi tusiweke mambo yetu binafsi, tuwe wazalendo."

Mwambe alidai aliangalia mahojiano ya Lissu katika kipindi cha Hardtalk na kuona

INAENDELEA UK. 8


## MPOKI AND ASSOCIATES ADVOCATES

### NOTICE OF SALE

**ALL THAT LANDED PROPERTY KNOWN AS PLOT NO 20 REGENT ESTATE DAR ES SALAAM CITY REGISTERED UNDER CT NO 52464 LO NO 191030 REGISTERED IN THE NAME OF ABLA ESTATE DEVELOPERS AND AGENCY COMPANY LIMITED**

1. **NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT,** under power contained in the mortgage deed dated 24th day of July 2008 in favour of **CRDB BANK PLC** and every other power enabling me to do so, **I MPALE KABA MPOKI, OF MPOKI AND ASSOCIATES, ADVOCATES** on behalf of the lender hereby advertise the sale of the captioned property owned by **ABLA ESTATE DEVELOPERS AND AGENCY COMPANY LIMITED.**

2. THE property is built on a plot with title deed issued on the 21st day January 2002 for a term of 33 Years, the title has an expired term of 33 years with effect from 21st day January 2002 to 21st day of January 2035, and the plot measures about 28750 square meters. Situate on the property is a 6 storey 3 Star running hotel, along Bagamoyo Road, about kilometres from the Airport, close to Makumbusho Village Museum, the hotel is close to several offices, historical centres and business premises.

   The Hotel known as **ALBA HOTEL APARTMENT** is a luxurious Hotel apartment with fully furnished one, two and three bedroom apartments with a fully equipped kitchen making an ideal destination for families or business travelers.

   The Hotel has a modern fitness centre, a large swimming pool and sauna.

   There is also a spacious conference hall with modern facilities a big parking place is also available.

3. **INTERESTED MEMBERS OF THE PUBLIC ARE INVITED** to submit bids for the purchase of the property.

4. Bids in sealed envelopes clearly marked "**BID FOR THE PURCHASE OF PROPERTY ON PLOT 20 REGENT ESTATE KINONDONI DAR ES SALAAM**", indicating the offer for the property with full address of the bidder shown and the same should be submitted so as to reach the undersigned on the address below before 16.00 hours on the 5th February 2019, Bids shall be opened on the 5th February 2019 ay 16.30 hours at the office mentioned below. Bidders are invited to attend during the event if they so wish.

5. Bidders should not that the information supplied herein is without liability to the seller as to its correctness. Independent valuation and inspection of the property is highly recommended.

6. The seller shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all.

7. The property is sold in a condition as it is.

8. It is a condition of the bid that bidders submit their bids accompanied by Bankers cheque in favor of CRDB BANK PLC of an amount equivalent to 10% of the bid price. For a successful bidder this amount shall be treated as advance payment. Unsuccessful bidders will have their bid commitment refunded in full without any deductions.

9. The successful bidder shall be bound to make a 25% down payment on the offer price within 4 days of the date of the award; and the balance shall be paid within 14 days thereafter

   **In the event the balance is not paid within 14 days the seller shall forfeit the down payment and the next highest bidder shall be awarded the option to purchase.**

10. Members of the public and or bidders who are desirous of viewing and or inspecting the property may do so subject to the appointment and prior consent of the seller agent on the address below:

    **ISSA BENDERA,**
    **COMRADE AUCTION MART,**
    **P.O. BOX 61508,**
    **DAR ES SALAAM,**
    **TANZANIA.**
    **PHONE NO 0758-212728,0623-212728**

11. Bids mentioned in paragraph 4 hereinabove should be addressed to the address below:

    **MPALE KABA MPOKI**
    **MPOKI AND ASSOCIATES, ADVOCATES,**
    **NO 4 REGENT STREET, OFF CHATO STREET,**
    **NEAR SUNRISE PRIMARY SCHOOL,**
    **P.O. BOX 14232,**
    **DAR ES SALAAM.**
    **PHONE: 0773-187777, 0715-187777**

215022002

# Wazazi wasiopeleka watoto shule sasa kupelekwa kortini

**Na Futuna Seleman,** KIBITI

SERIKALI wilayani Kibiti mkoani Pwani, imewataka wazazi walio-waandikisha watoto wao kujiunga na darasa la kwanza na waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza, kuripoti katika shule waliozochaguliwa vinginevyo watafikishwa mahakamani.

Mkuu wa wilaya hiyo, Gullam-Hussein Kiffu, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe baada ya kuzindua ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo, Kata ya Bungu, Kibiti mkoani Pwani.

"Kila mtoto ana haki ya kwenda shule, elimu bure watoto wote wapelekwe shule mzazi atakayemkataza au kumtumikisha, kumficha mtoto hatua stahili zitachukuliwa dhidi yake hatutakuwa na msalie katika hilo," alisema Kiffu.

Alisema kuna tabia imejengeka kwa baadhi ya wazazi, watoto wanapofaulu na kuchaguliwa kujiunga na shule za sekondari kuwakataza ili waolewe mapema na hao wadogo kuwatumikisha kazi za nyumbani au biashara za barabarani.

Akizungumzia ugawaji wa vitambulisho, alisema wajasiriamali wadogo 500 wamejiandikisha na Kata ya Bungu pekee imeongoza kwa kuwa na wajasiriamali wengi ikilinganishwa na kata nyingine 19 zilizomo ndani ya wilaya hiyo.

"Hongereni sana Bungu mmeongoza kujiorodhesha kwa wingi na wote mmehakikiwa mna sifa za kupata vitambulisho leo tutagawa vichache vya mfano, wengine mtachukua kupitia kwa watendaji kwenye maeneo yenu," alisema Kiffu.

Alisema utaratibu wa utoaji wa vitambulisho hivyo hautatolewa kiholela bali utasimamiwa na watendaji wa vijiji, kata kwa kushirikiana na watumishi wa halmashauri ili kudhibiti wasiokuwa na vigezo.

Kwa upande wao baadhi ya wajasiriamali wadogo walionufaika na vitambulisho hivyo kwa nyakati tofauti, walipongeza utaratibu wa vitambulisho kuwa haukuwa na urasimu.

"Tunamshukuru mheshimiwa Rais vitambulisho hivi vitatusaidia tusibughudhiwe tusimwagiwe biashara zetu sisi wananchi wanyonge tunamshukuru sana Magufuli kwa kutujali wananchi wa vipato vya chini," alisema Juma Ngondaye, aliyenufaika na vitambulisho hivyo.

Mamalishe, Salama Jabir, alisema kitambulisho hicho kitamaliza kilio kwa kinamama kumwagiwa vyakula vyao bila utaratibu na kumaliza vitendo vya rushwa kutozwa faini bila utaratibu.

"Tuna uhakika kufanya biashara kwa uhakika kwa kweli tunamwombea dua Rais wetu aendelee kuwapo madarakani ametusaidia sana, msaada si lazima mtu akupe pesa, kwa hili tunashukuru ametuondoa kwenye manyanyaso," alisema Salama.



Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mhandisi Omary Nundu (kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa duka jipya la TTCL, lililoko katika makutano ya Mtaa wa Mafia na Msimbazi, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Waziri Kindamba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kortini kumwita Rais mwizi

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA, Henry Munisi (30), mkazi wa jijini Mbeya, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka ya kuchapisha taarifa za uongo kwa njia ya mtandao kumwita Rais Dk.John Magufuli mwizi.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally. Alisomewa mashtaka na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Patrick Mwita.

Katika mashtaka hayo, Mwita alidai kuwa Desemba 28, mwaka jana jijini Mbeya, alichapisha taarifa za uongo kuhusu Rais.

Upande wa Jamhuri ulinukuu taarifa hiyo kupitia ukurasa wa Facebook wa Munisi kwamba, "Jinsi Magufuli alivyochota Sh. trilioni 1.5 za ATCL akitumia ujanja wake wa kuleta ndege ili atuibie," alinukuliwa taarifa hiyo. Mshtakiwa alikana mashtaka hayo.

Hakimu Ally alimtaka mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua za taasisi ya kuaminika watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. 500,000 kila mmoja.

Hata hivyo, alishindwa kutimiza masharti hayo na amerudishwa rumande mpaka Februari 6, mwaka huu, kesi itakapotajwa.

# Mmoja afariki dunia, watatu wafukiwa na kifusi mgodini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MTU mmoja amefariki dunia na wengine watatu kufukiwa na kifusi katika machimbo ya dhahabu ya Nyangalata, Kahama mkoani Shinyanga.

Akizungumza kwa njia ya simu jana, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimba Madini wa Mkoa wa Shinyanga, Hamza Tandiko, alikiri kutokea ajali hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita katika machimbo hayo chanzo kikielezwa kuwa ni ardhi kutitia katika moja ya miduara ya mgodi huo.

Tandiko alisema kutitia kwa ardhi katika duara hilo kumetokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika msimu huu na hakuna sababu ya shughuli ya kibinadamu inayoweza kuwa chanzo.

"Ni kweli kuna ajali ya shimo moja. Ardhi yenyewe tu ilititia na mtu mmoja amepoteza maisha na wengine wamefukiwa na kifusi kitu ambacho hatukukitarajia. Hatuna sababu kwamba labda pengine ajali imetokea kwa uzembe labda mlipuko au hapakujengwa vizuri," alisema.

Mmoja wa mashuhuda, ambaye ni manusura wa ajali hiyo, Malimi Magembe, alisema yeye na wenzake watatu walikuwa chini ya duara hilo wakati linatitia na mmoja wao alipata mshtuko na kuteleza kwenda chini hatimaye akafariki dunia.

"Wakati wa kutitia hilo shimo nilikuwamo na wenzangu. Mwenzetu mmoja alipata mshtuko baada ya kuona hiyo hali inatoka na akadondoka chini. Mwenzangu mmoja akaja upande wangu ndipo tuliokolewa na mwenzetu tukamwacha mle ndani akiwa amefariki dunia," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Simon Haule, alithibitisha kupokea taarifa za ajali hiyo na jitihada za kuwaokoa wengine watatu waliofukiwa chini zilikuwa zinaendelea kwa kushirikiana na wataalamu kutoka mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu.

"Kuna duara namba 2A, 3A,4A sasa kuna maduara mawili yako jirani, baada ya ardhi kutitia, kwenye duara moja walikuwamo watatu, wawili walitoka salama na mmoja alijirusha kwa kamba kwenda chini na akapoteza maisha ila kwenye duara lingine ambalo linadaiwa wako watatu tunafanya juhudi kuwaokoa.

Kipindi hiki cha mvua udongo umetepeta unakuwa laini ni rahisi kutitia, hivyo wananchi wachukue tahadhari kupitia wataalamu wa madini," alisema.

Wataalumu wa mgodi wa Bulyanhulu, kwa mujibu wa Kamanda Haule, wako katika eneo hilo na mitambo mikubwa na kwamba kinachofanyika kwa sasa ni kuchimba mashimo hayo kwa kuwa ni marefu.

Alisema watakapofika chini kiasi watawachia wachimbaji kuendelea kufukua kwa sababu eneo hilo ni kubwa kwa kuchimba mchanga huo.

Ajali za wachimbaji kufukiwa na machimbo, hususan migodi midogo, zimekuwa zikitokea kila mara katika kipindi cha mvua, hali inayoelezwa kusababishwa na udongo kutohimili shughuli zinazofanyika tofauti na kipindi cha kiangazi.

HABARI KITAIFA

# Gugai arudi mahabusu hadi Februari 5

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya utakatishaji fedha na kumiliki mali zisizolingana na kipato chake, dhidi ya Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai na wenzake watatu hadi Februari baada ya hakimu anayeisikiliza kuwa na udhuru.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba na jana ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Wilbard Mashauri.

Wakili wa Serikali, Vitalis Peter, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, lakini hakimu anayeisikiliza amepata udhuru na upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kusikilizwa.

Hakimu Mashauri alisema kesi hiyo iko mbele yake kwa ajili ya kutajwa kwa sababu hakimu aliyepangiwa kuisikiliza amepata udhuru, mahakama hiyo itasikiliza Februari 5, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Katika kesi ya msingi, Gugai na mwenzake, wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zisizoendana na kipato chake pamoja na kughushi mikataba ya mauziano ya viwanja katika maeneo mbali mbali.

Katika shtaka la kumiliki mali zisizoendana na kipato chake, mshtakiwa Gugai anadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Januari 2005 na Desemba 2015, akiwa ofisa wa umma ameajiriwa na Takukuru alikutwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake cha awali na cha sasa.



Mkuu wa Rasilimali Watu wa Zantel, Joan Makwaia Kazimoto, akiongea na wafanyakazi wakati wa mafunzo ya kujenga timu kazi bora, ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kufanikisha malengo ya mwaka ya kampuni katika kipindi cha mwaka huu, walipokutana katika hoteli ya Ndoto Polepole wilayani Bagamoyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo halmashauri mikononi mwa Takukuru

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Tanga, imeanza kuwahoji watendaji wa idara mbalimbali katika halmashauri zote za mkoa huu, ambazo zimeshindwa kutekeleza kwa wakati miradi ya maendeleo.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Tanga, Christopher Mariba, alisema hayo juzi, alipokuwa akitoa taarifa ya tathmini ya Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, mbele ya waandishi wa habari ofisini kwake.

Mariba alisema katika kipindi hicho, taasisi hiyo imebaini uwapo wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo imegharimu fedha nyingi za wananchi pasipo kuendelezwa au kumalizika kwa wakati.

Alisema kutokana na hali hiyo, Takukuru imeanza kuwahoji watu wote ambao wanahusika na miradi hiyo.

"Takukuru Mkoa wa Tanga kuanzia Januari 21, imeanza kuwahoji watendaji ambao tunaamini wanahusika na miradi hiyo ya maendeleo ambayo haijatekelezwa ipasavyo na kwa wakati," alisema Mariba.

Alisema miradi mingi ambayo watendaji wake wanahojiwa, imeanzishwa kwenye uongozi wa serikali ya awamu ya tano katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 na haijamalizika kwa wakati au kutekelezwa kabisa na miradi hiyo ingia kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, huku miradi michache ikiwa ilianzishwa na serikali ya awamu ya nne.

Mkuu huyo aliwataka viongozi wote wa Mkoa wa Tanga, hasa wakurugenzi wa halmashauri kuwa makini na kutoa ushirikiano, kwa kuwa kuna wakati watahitaji nyaraka za miradi hiyo ambayo imetelekezwa au kusuasua utekelezaji wake.

# Bunge lataka utatuzi wa vikwazo miradi hifadhini

**Na Lusungu Helela**, IRINGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii, imeishauri serikali kuangalia namna ya kuyaweka pembeni au kubadilisha ramani ya maeneo ambayo yanaonekana kuwa kikwazo katika utekelezaji wa mradi wa kukuza na kuendeleza utalii kusini (Regrow) ili ukamilike kwa wakati.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Nape Nnauye, alisema hayo juzi katika kikao cha majadiliano kati ya wadau wa sekta ya utalii na kamati hiyo kilichofanyika katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha mkoani Iringa.

Alisema Pori la Akiba la Selous limeonekana kuwa linapigiwa kelele kutokana na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Mto Rufiji, maarufu kama Stieglier's Gorge. Kutokana na hali hiyo, alisema: "Hili eneo tunaweza tukabadili ramani au kuliweka pembeni, ili maeneo yale ya mradi ambayo hayana tatizo utekelezaji wake ukaendelea, mradi huu unavyozidi kuchelewa kutekelezwa, ndivyo thamani ya fedha iliyokopwa inazidi kupoteza thamani yake." Alisema kutoa Selous yote si sawa, lakini inaweza kuchorwa ramani mpya kuhusu pori hilo kwa vile mvutano huo unaweza kuchukua miaka mingi hadi kufikia mwafaka kati ya serikali na Benki ya Dunia. Nape alisema licha ya kuwa mkopo huo si msaada, mkopeshaji ana haki ya kujua fedha zake zitarudishwaje na pia hazimletei mgogoro na watu wengine. Aidha, alisema uamuzi huo wa serikali ya kuamua kuchora ramani upya kwenye maeneo yenye matatizo, kutatoa fursa kwa utekelezaji wa mradi mingine katika ukanda wa Kanda ya Ziwa na kanda zingine ili kutimiza azima ya serikali ya kukusanya mapato yatokanayo na utalii.

Katika hatua nyingine, Nape aliishauri wizara kuangalia upya ushirikishwaji wa wadau ikiwamo sekta binafsi na jamii ya juu ya mradi unaotekelezwa kutokana na malalamiko yanayotolewa kuwa hawashirikishwi katika mchakato wa mradi huo. Akijibu hoja za wadau wa utalii na za wajumbe wa kamati hiyo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema mradi wa Stiegler's Gorge si kikwazo katika kuutekeleza mradi huo. Kanyasu alisema hata Benki ya Dunia haina kipingamizi katika utekelezaji wa mradi huo, bali kuna baadhi ya mambo katika mradi ndiyo yamechangia mkopo huo kuchelewa kutekelezwa ikiwamo ujenzi wa viwanda vya ndege ndani ya hifadhi za taifa.

Alisema baada ya kupitia upya mradi huo, wizara imegundua baadhi ya vitu haviko sawa, ndivyo vimesababisha kuleta mvutano ambayo bado mazungumzo yanaendelea hadi sasa.

Naibu Waziri alisema mradi wa Regrow ni mkubwa na kabla ya kuuanza, serikali iliajiri wataalamu kwa ajili ya kufanya utafiti ambao uligharimu fedha nyingi na ulishirikisha watu wengi kwa ajili ya kutoa maoni.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitendo hivi kwa wanafunzi ni aibu

**MMOMONYOKO** wa maadili ambao umekuwa ukilalamikiwa sana kutokana na kushika kasi katika jamii yetu, sasa umeanza kuathiri wanafunzi.

Haijulikani hali hiyo inatokana na nini, lakini sababu iliyo wazi ni kuwa jamii husuan wazazi na walezi wengi wanashindwa kutimiza wajibu wao wa kuwa karibu na watoto pamoja na kuwapa malezi mazuri.

Wajibu wa wazazi na walezi ni kuwafuatilia watoto nyumbani, maeneo wanayokwenda kucheza pamoja na shuleni wanaposoma, kuhakikisha kwamba watoto wao wanafuata na kuzingatia maadili mema. Inapotokea wazazi na walezi wakawa mbali na watoto, ni rahisi kuwafanya watoto kutenda mambo ambayo yanakwenda kinyume cha maadili, hivyo kuathirika kwa kiasi kikubwa.

Tumekuwa tukishuhudia athari kadhaa za watoto waliokosa malezi ya wazazi na walezi. Kwa mfano, watoto wa mitaani na wengine wanaoishi katika mazingira hatarishi ni zao la kukosa malezi bora ya wazazi na walezi.

Zimeripotiwa taarifa za kushtua na kusikitisha kutoka Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, hukusiana na wanafunzi wa shule kujihusisha na vitendo vinavyokwenda kinyume cha maadili.

Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mkuranga, umesema kwamba imebaini kukithiri kwa vitendo vya kulawitiana kwa watoto wa kiume katika baadhi ya shule zilizopo wilayani humo.

Kufuatia hali hiyo, kamati hiyo imewataka wazazi, walezi na wadau wa elimu wilayani humo kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao. Hayo yalibainika katika kikao cha wadau wa elimu kilichokuwa kikijadili changamoto za elimu wilayani humo, ushauri mapendekezo ya nini kifanyike kutatua changamoto zinazoikabili wilaya.

Kikao hicho kiliitishwa na Serikali ya Wilaya ya Mkuranga chini ya Mwenyekiti wake, Fillberto Sanga, kwa kuwashirikisha wadau wa elimu wakiwamo walimu, waratibu kata elimu, watendaji, madiwani viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa na watendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Ni dhahiri kwamba pale watoto wanapojiingiza katika vitendo hivyo, hawawezi kutilia mkazo masomo, hivyo kushuka kitaaluma na hatimaye kufeli mitihani.

Aidha, watoto wanapojiingiza katika vitendo hivyo mwishowe wanapata athari nyingine yakiwamo magonjwa ambayo yanaweza kuathiri sana afya zao.

Kama kamati ya ulinzi na usalama imelibaini tatizo hilo bila shaka limeshaathiri watoto wengi kwa njia mbalimbali, hivyo kilichobakia ni kuchukuliwa kwa hatua za haraka kulikomesha ili kuwalinda watoto wetu. Kwa kuanzia, wazazi na walezi wanapaswa kurejea katika mstari kwa kutimiza wajibu wao wa kuwafuatilia kwa karibu watoto wao pamoja na kuwapa malezi bora.


Wazazi na walezi ndio wenye jukumu la kwanza la kuwafundisha watoto maadili mema badala ya kuliacha jukumu hilo kwa walimu shuleni. Walimu wajibu wao mkubwa ni kuwapa taaluma na kuwasaidia wazazi na walezi kwa kuwafuatilia na kuwarekebisha kimaadili watoto hao.

Hata hivyo, walimu nao hawanabudi kuzingatia maadili kwa kuwa kuna malalamiko kuwa baadhi yao wanakiuka madili na kuchangia wanafunzi kujiingiza katika vitendo vikavyokiuka maadili. Kwamba baadhi ya walimu (wa kike na kiume) wanajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, kitendo ambacho licha ya kukiuka sheria na maadili, pia kinatoa picha mbaya kwa wanafunzi na jamii nzima.

Kinachotakiwa sasa ni wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa kuwapa watoto malezi bora sambamba na kuwafuatilia kwa karibu. Kwa upande wa walimu, wawe mfano mzuri kwa wanafunzi kimaadili pamoja na kuwafuatilia wanafunzi ambao wanaonyesha dalili za kujihusisha na vitendo viovu na kuwaathiri, ikiwamo kuwa watoro.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Uchungu wa mshikaki ulivyo, bodaboda inapopata ajali

**USAFIRI** wa bodaboda upo takribani kila kona ya nchi na umekuwa ukitumiwa na watu mbalimbali.

Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambako bodaboda hizo zilianza mbali zaidi, nikiutaja mkoa jirani wa Kagera hasa mjini Bukoba. Darasa lao kubwa kupata ujuzi huo, waliutoa nchi jirani, Kagera ilikopakana nako.

Usafiri wa bodaboda umekuwa ukitumiwa na watu mbalimbali ukiwawezesha watu kufika kwa urahisi katika maeneo waendayo, kwa kuwa haupotezi muda katika foleni, hasa katika maeneo ya mijini.

Usafiri huo umekuwa ukitumiwa na baadhi ya wazazi kwa kuwapeleka watoto shule, kutokana na wengi wao kushindwa kulipia usafiri wa mabasi ya shule.

Katika kufuatilia, nimebaini jambo moja kwamba madereva wanaoendesha bodaboda, wengi hawana elimu inayojitesheleza kwa ajili ya kutumia vyombo hivyo.

Serikali nayo imekuwa ikizungumzia hilo kila mara, kwamba kila anayetumia usafiri wa aina yoyote, ni lazima azingatie sheria itakayomwezesha kufika safari yake salama, katika sehemu aendayo.

Kuna baadhi ya watu wanaovunja sheria kupitia vyombo vyao na wanapokamatwa, wanajihisi sheria imewaonea, wakati katika ukweli si sahihi, bali inakuwa kinyumne chake.

Mtu anapoambiwa anaanza safari yake katika chombo cha moto, baadhi ya mambo ya msingi kama vile kufunga mkanda yanakuwa ya kuzingatia.

Pia, hata wale wenye watoto wanatakiwa wawaweke katika viti vyao, lengo ni kuwasuru na uwezekano wa madhara safarini, hasa pale ajali inapotokea.

> **Pia, hata wale wenye watoto wanatakiwa wawaweke katika viti vyao, lengo ni kuwasuru na uwezekano wa madhara safarini, hasa pale ajili inapotokea.**

Lakini ikiangaliwa, katika magari binafsi, baadhi yake hawazingatii hilo, watoto wao wanakalishwa kwenye viti vya mbele na hawana vizuizi vyovyote, jambo linalozaa hatari kwamba hata inapotokea ajali, mtoto huyo kupona ni shida kubwa.

Katika upande wa pili wa usafiri wa bodaboda, anapobebwa abiria, kunadai kuwapo kwa kofia ngumu mbili. Lakini, cha kushangaza ni kwamba unakuta baadhi ya bodaboda hazizingatii hilo na wanaishia kufanya watakavyo.

Unakuta abiria wapo watatu katika bodaboda na aliyevaa kofia ngumu ni dereva pekee, je, ajali inapotokea nani wa kulaumiwa?

Kwa nini sheria tunazivunja wenyewe, wakati tunajua bodaboda moja inabeba mtu mmoja?

Bila ya kufuata sheria za usalama barabarani, ajali hizi za bodaboda zitaendelea kusumbua na kuifanya serikali iingie gharama kubwa kuwahudumia majeruhi, ikiwamo matumizi makubwa ya damu, huku nguvu kazi bora ya umma ikipotea.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kimataifa Masuala ya Usalama Barabarani, Fotunatusi Sokoni, anatoa takwimu za ajali za pikipiki katika miaka miwili iliyopita.

Anazitaja takwimu; mwaka 2016 kulitokea jumla ya ajali 2,953 za pikipiki zilizosababisha vifo vya watu 990 na majeruhi 1,997.

Sokoni anasema, mwaka 2017 kulitokea jumla ya ajali 1,584 zilizosababisha vifo 763 na majeruhi 1,224.

"Ukiangalia mwaka 2016 na 2017 kuna tofauti ya ajali 1,019, yaani zilipungua kwa kiwango cha asilimia 22.9 na waliojeruhi ilikuwa ni pungufu ya watu 773 katika kipindi hicho," anasema.

# Kero tiketi za daladala

**Mhariri,**

*NILIWAHI kusoma katika gazeti hili, malalamiko ya msomaji na abiria mwenzangu wa daladala, kuhusu adha wanayoipata kuhusiana na tabia ya makondakta wa daladala kutotoa tiketi.*

*Kupitia jukwaa hilo la habari, nami nawasilisha hoja ya malalamiko inayoendeleza malalamiko kwa makondakta, hawatupatii tiketi.*

*Mara nyingi hata ukidai tiketi hiyo inakuwa mtihani mkubwa sana, kiasi cha kwamba inaangukia katika ugomvi.*

*Ni tabia inayotawala zaidi hasa kwa magari madogo aina yao Toyota Hiace na yenye ukubwa wa kati, Toyota Coaster.*

*Mara zote unapopanda magari hayo unakuwa mtihani mkubwa kwa abiria unapodai tiketi. Unaangukia katika msuguano na aina fulani ya ugomvi.*

*Pia, katika nyakati za mchana nayo ni tabia iliyojikita katika daladala za jijini Dar es Salaam, nikitoa mfano na zile zinazofanya safari zake kati ya Makumbusho na Segerea, ambako nauli ni Shilingi 450, lakini makondakta wanadai Shilingi 500 na wanakuwa wagumu kutoa chenji.*

*Hiyo ni tofauti sana na ratiba ya mabasi yanayoendesha huduma zao kati ya Gongolamboto na Posta ya Kivukoni, ambako daima tozo zake ni hizo hizo, Shilingi 450.*

*Mara zote makondakta hawadai ziada na inapotokea hata abiria akitoa Shilingi 500, kondakta anamrudishia abiria Shilingi yake 50 bila ya mgogoro, huku akimpatia chenji.*

**Hamadi Gomenyi**
**Tabata Magengeni,**
**Dar es Salaam.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Tumekuelewa DC Jokate Mwegelo, hutanii kuhusu mimba za mabinti

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, Jokate Mwegelo, anasema hatawavumilia watendaji na wazazi wanaowaficha 'mafataki' wanaowapa mimba wanafunzi na kusababisha kukosekana ushahidi wa kuwatia hatiani.

Tahadhari yake ni kwamba watakaobainika kuharibu mambo watachukuliwa hatua kali za kisheria, bila ya kujali mamlaka na vyeo walivyo navyo ndani ya chama na serikali.

Inasemekana kwamba, kwa kiasi kikubwa tatizo la mimba linachangiwa na wazazi, watendaji wa vijiji na kata kwa kutotoa ushirikiano, ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika, badala wanaoshiriki kupoteza ushahidi.

"Tatizo kubwa liko kwa wazazi na watendaji, sasa nawaambia tumekaa na viongozi wenzangu wa wilaya tumesema hatuko tayari tena kuvumilia suala hili," anasema Mwegelo.

Ni kauli yale alipopokea magodoro 20 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Maneromango, yalitolewa na wabunge wawili wa viti maalum wa mkoa wa Pwani.

Vilevile, kuna taarifa ya Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Abdul Maulid, inayoonyesha kuwa wanafunzi 235 wa shule za msingi na sekondari mkoani Pwani, wamepata mimba katika kipindi cha mwaka 2018.

Ofisa huyo alitoa taarifa hiyo hivi karibuni katika kikao cha ushauri cha mkoa na kufafanua kuwa wanafunzi 155 ni wa shule za msingi, 80 wa sekondari.

Natambua juhudi mbalimbali zinachukuliwa na serikali, kwa ajili ya kutokomeza mimba kwa wanafunzi, lakini inawezekana juhudi hizo zikakwamishwa na baadhi ya watu ambao DC Mwegelo anawataja.

Siyo jambo jema mzazi au kiongozi kushirikiana na mtu anayeharibu ndoto za mtoto wa kike, kwa kumpa ujauzito eti kwa sababu ya kupewa chochote.

Kuna sababu nyingine zinazotajwa, kuhusu mimba hizo kuwa ni kutokana na umaskini wa kipato cha wazazi, lakini watambue kuwa hiyo ni njia haramu ya kujitafutia mali, ni vyema wakabadilika na kutumia njia halali.

Watoto wa kike wanapaswa kuachwa watimize ndoto zao, badala ya kuwaacha wapate mimba na kisha kuwaficha, ili wahusika wa mimba hizo wasikamatwe.

Ikumbukwe kwamba, idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo, kwa sababu ya mimba katika shule za msingi na sekondari nchini, imekuwa ikizidi kuongezeka, hali inayotishia maendeleo ya elimu nchini.

Takwimu zilizokwishatolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Watoto toka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Margaret Mussai, zinaonyesha kuwa idadi hiyo imeongezeka kutoka takribani 3,000 kwa mwaka 2013, hadi wanafunzi 5,033 mwaka 2016.

Anatoa takwimu hizo kwa wanahabari, alipozindua kampeni ya kupiga vita mimba za utotoni na rushwa mkoani Dodoma na akafafanua kuwa wanafunzi wengi walioacha masomo ni wa ngazi ya sekondari, ambao ni zaidi ya 4,033, huku wa shule za msingi ni 600.

Jokate anafafanua kwamba, kutokana na kuongezeka wimbi la kuacha masomo sababu ya mimba, wizara hiyo ilizindua Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kuendesha kampeni nchi nzima kukomesha vitendo hivyo.

Anasema, katika kampeni hiyo ya miaka mitano itamalizika mwaka huu wa 2019, lakini serikali itafanya tathmini na kupima matokeo mwaka 2022, kuona kama tatizo hilo limepungua au bado linaongezeka na hatua gani za makusudi zichukuliwe kukomesha.

Mussai anasema, utafiti uliofanywa na wizara hiyo imebaini watoto wengi wanapata mimba wakiwa shuleni kutokana na umaskini na umbali kutoka nyumbani hadi shuleni, unaowafanya waendeshaji bodaboda, bajaji na daladala, wanautumia kama mwanya wa kuwahadaa kuwapa lifti na hatimaye kuwaingiza katika mapenzi.

Anasema, wanaopata mimba kwa ukatili unaofanywa nyumbani na ndugu, jamaa na marafiki wanafikia takribani asilimia 60, huku asilimia 40 zinazobaki watoto wanafanyiwa ukatili kutoka shuleni, baadhi ya walimu na viongozi wengine.

Kitaifa ni kwamba, wasichana 27 kati ya 100 ndio wanaopata mimba wakiwa na umri chini ya miaka 18 na kitendo ambacho ni hasara kwa taifa.

Wito wake ni kwamba anawataka wazazi, walimu, viongozi wengine katika maeneo yao, warudi kwenye maadili, wawalee watoto na kuwaonya athari za mimba wakiwa shuleni, kwa kuwa zinafupisha na kukatisha ndoto zao za baadaye.

Kwa wenye masikio wasikie na kuzingatia wito wa mkurugenzi huyo na hata wa DC Mwegelo, kwa sababu ni kweli wazazi na viongozi wanaoshiriki kuficha watu wanaowapa mimba wanafunzi hawavumiliki.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



## Mtoto afa kwa kuliwa na panya

INATOKA UK. 3

Mama huyo alisema ilipofika saa tano kamili usiku, alipitiwa na usingizi mzito na alishtuka majira ya saa 10:00 alfajiri kwa lengo la kumbadilisha nguo kama amejisaidia kama ambavyo alikuwa akifanya siku zote.

Alisema alipowasha kibatari, wakati akimyanyua mtoto katika kitanda, aliona tofauti na siku zote huku mtoto akiwa amelegea na alipojaribu kumnyonyesha, alikuwa bado amelegea na alipomchunguza vizuri katika mguu wake wa kushoto aliona umeliwa nyayo, kisigino na goti mfupa unaonekana nyama na ngozi za mguu hakuna.

Haule alisema alisema ilipofika asubuhi, aliita watu akiwamo mwenyekiti wa kijiji cha Kwabada, Joseph Thomas, na kugundua mtoto huyo ameshafariki dunia. Ofisa mtendaji wa kijiji cha Kwabada,

Anneth Mkonge, alisema tukio hilo tayari limeshaipotiwa polisi na utaratibu wa uchunguzi unaendelea kufanyika.

# Waziri aelekeza viongozi wanaokiuka viapo kubanwa

**Na Mwandishi Wetu**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetakiwa kuwachukulia hatua kali za kinidhamu viongozi wanaokula kiapo cha ahadi ya uadilifu na kutoa tamko la rasilimali na madeni, lakini wanashindwa kutekeleza kiapo hicho.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, wakati akizungumza na watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, alipofanya ziara ya kikazi makao makuu ya ofisi hizo jijini Dodoma, yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji, kufahamu kwa kina majukumu ya sekretarieti na kujiridhisha namna inavyotekeleza wajibu wake.

Mwanjelwa alisema, baadhi ya viongozi wamekuwa wakila kiapo cha ahadi ya uadilifu na kusoma tamko la rasilimali na madeni, lakini maisha na tabia zao ni tofauti kabisa na viapo wanavyoapa, hivyo ameisisitiza Sekretarieti ya Maadili kutumia sheria kuwawajibisha viongozi wa namna hiyo kwa kuwa ni mzigo kwa taifa.

Mwanjelwa alisema viapo na matamko ni lazima viendane na uhalisia, hivyo ameitaka sekretarieti hiyo kufanya ufuatiliaji na kuchukua hatua bila uwoga wowote kwa kiongozi anayeenda kinyume kwa sababu kiongozi wa namna hiyo anakosa sifa ya kuwa kiongozi bora.

Mwanjelwa alisema ni lazima kuunga mkono kwa vitendo jitihada za serikali za kupambana na viongozi ambao hawana maadili mema ili kuleta maendeleo kwa taifa.

Aidha, Mwanjelwa aliwataka watumishi wa sekretarieti hiyo kuishi na kufanya kazi katika maadili mema, ili wawe mfano kwa wanaowasimamia katika suala zima la maadili.

"Ni lazima maadili mema yaanzie kwetu sisi, ili tunapozungumza na kutoa elimu ya maadili kwa viongozi tuwe kioo kwa kuwa huwezi ukazungumzia maadili kwa viongozi kama wewe mwenyewe huna maadili, hivyo ni lazima kuonyesha mfano," Mwanjelwa alisisitiza.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Kamishna wa Sekretarieti, Jaji mstaafu Harold Nsekela, alisema, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi wa umma yeyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba masharti ya sheria ya maadili ya viongozi wa umma yanazingatiwa ipasavyo.

Jaji Nsekela aliyataja majukumu ya sekretarieti ni pamoja na kupokea matamko ya viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kuanzisha na kufanya uchunguzi wowote kuhusu ukiukwaji wa maadili yaliyotajwa na sheria, kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi na kufanya uhakiki wa tamko la rasilimali na madeni ya viongozi wa umma wanaotajwa na sheria.




Meneja Masoko na Biashara wa TBL na AB InBev Afrika Mashariki, Edith Bebwa (katikati), akimkabidhi ufunguo wa gari mkazi wa Arusha, George Issaya, wakati wa hafla ya kumkabidhi gari aina ya Renauld Kwid, aliyojishindia wakati wa promosheni ya TBL Kumenoga Tukutane Baa, iliyomalizika hivi karibuni. Hafla hiyo ilifanyika Ilala jijini Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa Huduma za Masoko wa TBL, David Tarimo. **MPIGAPICHA WETU**

# Bosi TIC ajitosa kumvaa Lissu

INATOKA UK. 3

alizidiwa uzalendo na mtangazaji wa kipindi hicho.

"Mwandishi alikuwa na uelewa wa mambo yanayofanyika Tanzania kuliko Lissu, mwandishi alionyesha mazuri anayoyajua, lakini Lissu yeye hayaoni hata moja, anampinga mwandishi ambaye hata siyo Mtanzania," alisema.

"Hii ilionyesha picha mbaya, yaani anaitangaza nchi kwa mabaya bila kujiuliza athari zake, huku akitaka kugombea mwaka 2020 kama wananchi wa Singida na chama chake wakimpa ridhaa, anataka agombee aikute nchi ikiwa chafu ambayo yeye anaichafua. "Anataka agombee aikute nchi haiaminiki... tuwe wazalendo kwenye mambo ya msingi unayasimamia kama nchi."

Mwambe alisema yapo mengi mazuri ambayo chini ya Rais Magufuli yametekelezwa ukiwamo ujenzi wa reli, barabara, umeme na madaraja.

Alisema TIC inahakikisha hata kama mtu hayupo serikali atumie nafasi aliyonayo kuitangaza nchi ili kuvutia uwekezaji na siyo kuichafua.

"Naomba mwandike vitu vizuri kuhusu nchi kwa sababu maneno huumba. Sisi siyo maskini, sema bado hatujageuza rasilimali tulizonazo kuboresha maisha ya watu," alisema.

Bosi huyo wa TIC pia alisema wanaendelea kuimarisha masuala ya kuvutia uwekezaji na kuimarisha zaidi ofisi zao za kanda, ili kuwahudumia wawekezaji na wananchi.

Alisema hategemei waziri mpya na katibu mkuu wake kuwa na kazi ya kutatua migogoro ya wawekezaji na taasisi za umma au na mamlaka za serikali, hivyo kuzitaka sekta zote zitimize wajibu wa kuhamasisha uwekezaji.

Alisema masuala ya uwekezaji yakiandikwa na kutangazwa vizuri, yanasaidia nchi kuvutia uwekezaji zaidi duniani.

## Udasa watishia kuingia mgogoro na serikali

INATOKA UK. 3

kutokupandishwa madaraja licha ya kukidhi vigezo.

"Kwa miaka mitatu mfululizo, wanataaluma wanaokidhi vigezo vya kupandishwa madaraja, hawapandishwa na wa miaka mingine waliopandishwa kwa kigezo cha kuhitimu masomo, hawajalipwa stahiki zao kwa miaka mitatu sasa," alisema.

"Wakati haki yao ikicheleweshwa, wamekuwa wakiendelea kupangiwa majukumu mazito yanayoendana na vyeo vyao vipya visivyo na mishahara wala motisha yoyote wanavyostahili.

"Huu si utaratibu sahihi hata kidogo na hatuwezi kuendelea kuvumilia kwa kuwa unashusha morali ya utendaji kazi kwa wanataaluma katika chuo kikuu na ni hatari sana katika uimara na uendelevu wa elimu ya juu nchini.

"Kimsingi, hatuko tayari kuona hali hii inaendelea kwa kuwa tunatambua athari zake ambazo zinaendelea kujitokeza waziwazi."

Alisema Udasa inaishauri serikali kufanyia kazi madai hayo ikiwamo kulipa malimbikizo yote ya fedha wanazodai kufikia mwishoni wa Februari.

"Serikali kupitia menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina, ilipe mara moja ifikapo mwisho wa mwezi Februari mwaka 2019 madai yote tuliyoyataja," alisema.

Aliongeza: "Serikali ianzishe utaratibu wa kuambatanisha malipo ya posho ya nyumba na mishahara yao ya kila mwezi kwa wanaostahili na Ofisi ya Utumishi iwapandishe mara moja wanataaluma wanaostahili vyeo vipya na ianze kuwalipa mishahara inayoendana na vyeo hivyo.

"Ni matumaini yetu kuwa serikali itaona haja ya kuufanyia kazi ushauri wetu na kuyalipa madai haya, kinyume cha hapo, serikali yenyewe itakuwa imetangaza mgogoro na wanataaluma.

"Mgogoro huo si tu utazidisha athari, bali utatulazimisha wana Udasa kuondoa nguvu moja baada ya nyingine katika yale tunayoyafanya ikiwa ni sehemu ya wajibu wetu kwa mwajiri."

# Rushwa ya mkaa yawapandisha kizimbani

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Katavi, imewapandisha kizimbani askari mgambo wawili wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya magunia matatu ya mkaa na fedha taslimu Sh. 20,000.

Watuhumiwa hao Lazaro Kambaulaya na Charles Kisauko walifikishwa mahakamani juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Mlele, Proscovia Niyongataile, na kusomewa mashtaka yanayowakabili.

Askari hao walikuwa wakitumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kukagua usafirishaji wa mazao ya misitu kwenye maeneo mbalimbali ya vizuizi vilivyoko katika Tarafa ya Inyonga.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, kuwa watuhumiwa hao walikamatwa baada ya Takukuru kupokea malalamiko kutoka kwa msiri wao ambaye alidai kuwa yeye na mwenzake wameombwa rushwa ya magunia matatu ya mkaa pamoja na fedha taslimu Sh. 20,000, ili wawaruhusu kusafirisha mkaa bila leseni na kibali cha maliasili.

Baada ya taarifa, ilidaiwa kuwa Takukuru ilianza kufanya uchunguzi kuhusiana na tuhuma hizo pamoja na kuweka mtego, hivyo kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao Januari 17, mwaka huu, baada ya kupokea rushwa kutoka kwa watu waliowaomba.

Kutokana na kukamatwa huko, watuhumiwa walifikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Baada ya kusomewa mashtaka, watuhumiwa hao walikana kuomba na kupokea rushwa, lakini walipelekwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana. Kesi hiyo itatajwa Februari 4, mwaka huu.



Gari likiwa limetumbukia kwenye mtaro baada ya kushindwa kukata kona katika Barabara ya Shekilango, eneo la Sinza Legho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSAL**

# Ujenzi ofisi wizara wamkuna Mabula

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameelezea kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa ofisi za wizara katika mji wa serikali ya Mtumba mkoani Dodoma.

Mabula alielezea hayo juzi alipotembelea mradi wa ujenzi huo unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambalo liko chini ya wizara yake.

Alisema kazi hiyo inakwenda kwa kasi na inatia moyo jambo linaloonyesha kuwa mradi mradi huo utakamilika katika muda uliopangwa.

Katika mradi huo, NHC kupitia kampuni yake ya ujenzi, inajenga ofisi za Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Fedha na Uchumi; Nishati, na Viwanda na Biashara.

Aidha, Mabula alielezea kufurahishwa na ufuatialiaji wa ujenzi wa ofisi hizo unaofanywa na wizara za Fedha na Uchumi, Viwanda na Biashara na kusema hatua hiyo inalifanya shirika hilo kufanya kazi kulingana na mahitaji ya wateja wake.

Alibainisha kuwa pamoja na changamoto ya kukatika umeme, NHC imejitahidi na kilichomfurahisha ni kuwapo vifaa vyote vya ujenzi kwenye eneo la ujenzi, jambo linalompa faraja kuwa hakuna kitakachokwamisha mradi kukamilika kwa wakati. Naibu Waziri alipongeza jitihada zinazofanywa na Rais John Magufuli za kuhamishia makao makuu ya serikali Dodoma na kubainisha kuwa hatua hiyo inatimiza ndoto ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Emma Lyimo, aliisifu NHC kwa kasi kubwa inayoendelea nayo kwenye ujenzi wa ofisi ya wizara yake na kubainisha kuwa pamoja na kuchelewa kuanza ujenzi, ana imani ujenzi utakamilika kwa wakati.

Naye msimamizi wa ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo la Makazi, Mhandisi Grace Musita, alisema ujenzi wa ofisi umefikia asilimia 75 na anatarajia utakamilika katika tarehe iliyopangwa kwa kuwa wamefikia hatua nzuri ya kukamilika.

# DC akerwa kasi ndogo urejeshaji wa mikopo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amesikitishwa na kitendo cha vikundi vya ujasiriamali mjini hapa, ambavyo vilipewa mikopo kwa ajili ya kujiiunua kiuchumi, kutorejesha kwa wakati.

Mboneko alibainisha hayo juzi alipotembelea na kukagua vikundi vya vijana na wanawake, vilivyopewa mikopo na Manispaa ya Shinyanga asilimia 10 kupitia fedha za mapato ya ndani.

Alisema anasikitishwa na taarifa kuwa baadhi ya vikundi hivyo kushindwa kupeleka marejesho.

Kwa mujibu wa Mboneko, fedha hizo zinatakiwa kurejeshwa kwa muda mwafaka ili vikundi vingine vipate mikopo na kujikwamua kiuchumi, lakini cha ajabu marejesho yamekuwa magumu mpaka kuanza kushikana mashati.

Kutokana na hali hiyo, mkuu huyo wa wilaya aliagiza vikundi ambavyo vimekuwa na matatizo ya kurejesha visipewe mkopo tena.

"Naombeni sana vikundi ambavyo mmeshapewa mikopo mzirejeshe fedha hizo ili vikundi vingine navyo vipewe. Wale ambao wamekuwa wagumu, naagiza wasije wakapewa tena mikopo hiyo sababu tutakuwa tunateketeza fedha bure na kuitia hasara serikali," alisema.

"Napenda pia kutoa pongeza kwa wanawake ambao wamekuwa wakijitokeza kuunda vikundi na kufanya shughuli za ujasiriamali na kuondokana na dhana tegemezi ambayo ilikuwa ikiwasababishia manyanyaso kutoka kwa waume zao," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa Kikundi cha Kusindika Uyoga, Kephuleni Nuhu, alisema walipata mkopo mwaka jana wa Sh. milioni 15 na wako watu 10, lakini wameshindwa kurejesha fedha hizo kutokana na kushindwa kuuza vizuri sababu ya kukosa soko kubwa na kuahidi mwaka huu watajitahidi kurejesha hata kidogo.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Shinyanga, Magreth Lyanga, alisema kwa mwaka jana wametoa mikopo kwa vikundi 14 vya wanawake vinane yenye thamani ya Sh. milioni 50.9 na kwa vijana sita vya Sh. milioni 47.

Hata hivyo, Lyanga alibainisha kuwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa wakati kinyume cha makubaliano.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya kimataifa ya kuhudumia shehena ya kontena bandarini (TICTS), Jared Zerbe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampuni hiyo, kuweka rekodi mpya ya kiwango cha kuhudumia kontena kufikia 592,000 kwa mwaka 2018, tofauti na kontena 501,690 kwa mwaka 2017. Kushoto ni Mkuu wa Rasilimali Watu na Ofisa Utawala wa kampuni hiyo, Ladislaus Prosper. **PICHA: JOHN BADI**

# Baba na mtoto wauawa kikatili kwa kupigwa risasi

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

KUNDI la watu wasiofahamika, mmoja akiwa amevalia sare inayofanana na jeshi, limewashambulia kwa risasi hadi kuwaua baba na mwanawe, wilayani Biharamulo, mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, amethibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kuwataja waliouawa kuwa ni mwanafunzi wa darasa la kwanza, Shule ya Msingi Nyabugombe, Mukiza Philibert na baba yake Philibert Kinyana.

Alisema mwanafunzi huyo alipigwa risasi mguu wake wa kulia, huku baba akipigwa rasasi ya kichwani na shingoni na kusababisha vifo vyao. Akielezea tukio hilo Kamanda Malimi alisema, lilitokea Januari 20, mwaka huu, majira ya saa 12.20 jioni wakati kundi hilo lilipisimamisha gari lililokuwa likiendeshwa na Kinyana aina ya Toyota Premio lenye namba za usajili T957CKJL na kuanza kuwashambulia kwa risasi kupitia kioo cha gari cha mbele.

Alisema kundi hilo lilikuwa na silaha za fimbo, huku mmoja aliyekuwa amevalia sare ya jeshi akiwa na silaha aina ya AK. 47.

Kamanda Malimi alisema Kinyana alipogundua watu hao hawakuwa na nia njema alikimbiza gari kuelekea msituni, lakini liligonga mti na kusimama kitendo kilichosababisha wahalifu hao kuwavamia na kuwapiga risasi hizo hadi kuwaua. Alisema kuwa baadhi ya watu kwenye kundi hilo walikuwa wakizungumza lugha ya Kinyarwanda na fimbo zao zilikiwa na asili ya nchi ya Rwanda.

"Aliposimama walianza kufyatua risasi mbele ya gari, Kinyana alianza kukimbia na kugonga mti hali iliyomfanya ashindwe kuendelea na safari," alisema.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni kulipiza kisasi kwa madai ya wizi wa ng'ombe. Katika tukio jingine Kamanda Malimi alisema, Januari 19, mwaka huu, Kata ya Kaisho, wilayani Kyerwa, Peter Ezekiel (27), amekutwa ameuawa na kukatwa sehemu mbalimbali za mwili zikiwamo sehemu za siri na mwili wake kuchomwa moto. Aidha, alisema kuwa katika Kijiji cha Ngararambe, Kata Nyakahura, wilayani Biharamulo, watu wawili mke na mume wakazi wa Ukerewe mkoani Mwanza, walikutwa wamefariki dunia wakiwa wamelala kwenye nyumba yao kwa kukosa hewa.

Alisema maelezo ya awali ni kwamba marehemu hao Mkono Selestine (51) na Leticia Gatawa (48), walikwenda wilayani humo kufanya shughuli za kilimo na kujenga nyumba ambayo haikuwa na madirisha ya kutolea hewa. Alisema nyumba hiyo ilikuwa imejengwa kwa muundo wa hema ndani walikuwa wanapika na kulala humo humo na kusahau kuzima moto.

# Insha kushindanisha wanafunzi vyuo vikuu

**Na Felix Andrew**

WANAFUNZI wa elimu ya juu nchini, wameshauriwa kushiriki katika mashindano ya insha ambazo zitawawezesha kuongeza uelewa na kipato.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Masoko wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Deborah Haule, wakati akielezea maendeleo ya shindano la uandishi wa insha ambalo taasisi hiyo imeandaa baadaye mwezi ujao.

Alisema mashindano ya insha yanasaidia sana kukuza uelewa na kuwawezesha washiriki kupata zawadi hasa kwa watakaoibuka washindi.

Alieleza kuwa, shirika hilo limekuwa likiwahamasisha wanafunzi wa vyuo vikuu nchini kushiriki katika shindano hilo.

Kauli mbiu ya shindano la insha mwaka huu ni umuhimu wa viwango katika kupambana na rushwa kwa ajili ya mageuzi endelevu ya Bara la Afrika.

Alisema hadi sasa maofisa wa shirika hilo wameshatembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) , Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo cha Usafirishaji (NIT) na Chuo Kikuu cha Mt Joseph, ambapo zaidi ya wanafunzi 300 walihudhuria.

Alidokeza kuwa mwitikio ni mkubwa na kuongeza kuwa wanatarajia kutoa zaidi elimu ya uhamasishaji ushiriki wa shindano hilo kwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Chuo Kukuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE).

Alisema dhumuni la shindano hilo la sita la insha ni kuongeza uelewa kuhusu madhara ya rushwa kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Bara la Afrika na pia kuangalia namna viwango vitakavyoweza kutumika kwa ajili ya kupambana na tatizo hilo.

Aliwataka wanafunzi wa elimu ya juu nchini kuwa mabalozi wazuri katika kueneza umuhimu wa viwango, ili kuliwezesha taifa kuingia katika uchumi wa kati ifikapo 2025.

# SAGCOT yapania mageuzi kilimo

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), kimejipanga kutoa mchango stahili wa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo kama sehemu ya kufanikisha ujenzi wa viwanda nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuelezea mikakati yake kwa mwaka 2019, Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, alisema kituo kitaunganisha nguvu kutoka sekta za umma na binafsi, ili kutia mchango katika maendeleo na ukuaji wa sekta hiyo muhimu.

"Kama wadau katika sekta ya kilimo, tutashirikiana na serikali pamoja na wadau katika sekta binafsi kufanikisha azima ya serikali ya Rais John Magufuli kuleta mageuzi makubwa katika kilimo, ili kuchochea ukuaji wa sekta ya viwanda," alisema.

Kirenga alisema mafanikio ambayo kituo hicho kimeshayapata kupitia kongani zake yatakuwa chachu katika kufanikisha malengo ya serikali katika kilimo.

"Ni ukweli usiopingika kuwa azima ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 itafikiwa kwa urahisi endapo uzalishaji na tija zaidi itapatikana katika sekta ya kilimo," alisema.

Kirenga alisema duniani kote malighafi nyingi zinazohitajika zinatokana na kilimo na Tanzania iko katika nafasi nzuri.

"SAGCOT ina imani kubwa na hatua zinazochukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwa zitazaa matunda," alisema na kuwaomba wadau wote katika sekta ya kilimo kushirikiana na kuunga mkono jitihada za serikali.

Kirenga alizungumzia pia ziara za Naibu Waziri wa Kilimo katika taasisi yake kuwa inaonyesha dhamira ya serikali kushirikiana na wadau wote kuijenga sekta ya kilimo.

Tayari kituo kina kongani tatu ambazo zipo hai ikiwamo ya Ihemi kwa mikoa ya Njombe na Iringa, Mbarali kwa mikoa ya Mbeya na Kilombero kwa wilaya zote katika Mkoa wa Morogoro.

Imefanikiwa kuwaunganisha wakulima katika kongani zake ikiwamo kuwajengea uwezo, mbinu za kilimo biashara na kuwaunganisha na wadau mbalimbali wa kilimo.

# TRA yatoa angalizo wanaofunga biashara bila kutoa taarifa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani Manyara, imewataka wafanyabiashara wanafunga biashara zao wahakikishe wanatoa taarifa kwa mamlaka hiyo pamoja na kulipia madeni vinginevyo wahusika wakifariki dunia wasimamizi wa mirathi watadaiwa.

Meneja wa TRA mkoani hapa, Joseph Mtandika, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu wafanyabiashara wanaofilisika na kuamua kurudisha namba zao za usajili yaani TIN na baadaye wakipata mtaji wanaanza upya biashara.

"Kwanza ni vizuri watu wafahamu kuwa mtu aliyefilisika, yaani, mtu aliyeingia mfilisi mahakama ndiyo inayotamka kuwa fulani ni mfilisi na mali zake ziuzwe," alisema.

Alisema wafanyabiashara hawatakiwi kusema wamefilisika na kurudisha namba zao za usajili wa kufanya biashara badala yake wahakikishe wamelipa madeni yao ndipo waache kufanya biashara.

Akitoa mfano, alisema, ofisi yake imeanza taratibu za kuchunguza watu watatu waliodai wamefilisika wilayani Kiteto na mmoja akiwa ameshafariki.

Alisema hata hivyo, watatakiwa kulipa kodi aliyokuwa anadaiwa kwa kuuza mali zake kama nyumba, kiwanja au gari au vyote na kama hawana mahakama itatoa maamuzi yake.

"Sisi watu wanaosema wamefilisika kabisa katika mkoa wetu tunao watatu kule Kiteto, tena mwingine amekwishafariki ila tutashughulika na wasimamizi wake wa mirathi na ikishindikana kabisa mara nyingine mahakama inaturuhusu kuwapeleka bungeni ili kuliomba Bunge litoe msamaha kuwa kweli wamefilisika," alieleza.

Alisema alitumia fursa hiyo kuwataka wateja wao kuwa waaminifu na wazalendo na wanapoacha biashara watoe taarifa ofisi za TRA, ili waweke kumbukumbu zao sahihi na kusitisha rekodi za biashara zake.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara wanaofilisika na kujidanganya kuwa watarudisha TIN namba na kuacha biashara kirahisi wawe na uhakika kuwa wamelipa madeni yao tofauti na hapo wakienda mikoa mingine kufungua biashara watakapoenda TRA kupata TIN mpya wakiweka vidole gumba vyao vitawabaini kuwa waliwahi kupewa TIN namba mkoa fulani, hivyo, watatakiwa kurudi alikotoka.



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wakipitisha rasimu ya mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 35.4 kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mkutano mkuu wa kijiji wamvua madaraka mwenyekiti

**Na Cynthia Mwilolezi,** MONDULI

MKUTANO Mkuu wa Kijiji cha Emirete, Kata ya Monduli Juu, wilayani Monduli, umemvua madaraka mwenyekiti wa kijiji hicho, Melusori Mollel, kwa madai ya kuhujumu sehemu ya ardhi ya kijiji hicho na kuwapa Kijiji cha Lendikinya.

Wakizungumza katika mkutano huo, uliofanyika juzi, wakazi wa kijiji hicho, walisema wanaungana na wajumbe wa halmashauri ya kijiji hicho ambao walikutana mwishoni mwa wiki iliyopita na kupiga kura ya kutokuwa na imani naye kutokana na masuala mbalimbali ikiwamo madai ya kushirikiana na halmashauri kuweka mipaka ya vijiji bila kuwashirikisha.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Monduli, Stephen Ulaya, alisema iwapo wananchi hao wana tuhuma dhidi ya kiongozi wao wanapaswa kufuata taratibu za kumfukuza kwa kutumia utaratibu uliomweka madarakani, ikiwa ni pamoja na kumpa nafasi ya kujitetea.

Mmoja wa wakazi hao, Namnyaki Saitoti, alisema wameamua kuungana na uamuzi huo wa wajumbe wa halmashauri ya kijiji kumvua madaraka wakimtuhumu kushirikiana na halmashauri kuweka mpaka wa kijiji bila kushirikisha wajumbe wenzake wala wananchi na eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 500 kuwapa kijiji hicho cha jirani.

Naye Jackson Ngokola, alisema wamesikitishwa na kitendo alichofanya mwenyekiti wao kusimamia eneo lililokuwapo kijijini hapo kugawanywa kwa kijiji kingine.

"Ni masikitiko Mollel kutugeuka na tunaungana na halmashauri ya kijiji kumteua mwenyekiti wa muda, ili tuendelee kufuatilia tatizo hili kwa kuwa ni muda mrefu hatumwoni.

"Alishiriki zoezi la kuweka mipaka wakati sisi hatujui lolote, mpaka uliopitishwa siyo mpaka halali ambao ulikuwapo katika ramani ya awali ya kijiji," alisema. Kwa upande wao wajumbe wa halmashauri ya kijiji hicho, Edward Laizer na Mboya Kayezi, walidai kikao cha kumpigia Mollel kura ya kutokuwa na imani kilifanyika Jumamosi iliyopita baada ya kuona kiongozi wao kutotekeleza majukumu yake ipasavyo.

Laizer alidai katika kikao hicho kilichohudhuriwa na wajumbe 17, wajumbe wote walipiga kura za hapana za kutokuwa na imani naye na wakamteua Meliyo Lukumay kuwa mwenyekiti wa muda wakati wanasubiri uchaguzi ufanyike.

Wananchi wa vijiji hivyo viwili wanagombea eneo lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 530, ambalo awali lilikuwa likitumiwa na wawekezaji, (TBL), katika kata hiyo iliyopo wilayani Monduli.

# Mkurugenzi ataka watumishi kuacha alama na kumbukumbu nzuri

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, amewataka watumishi wa serikali na jamii, kutimiza wajibu wao ipasavyo ili waache alama na kumbukumbu nzuri hapa duniani.

Myenzi, aliyasema hayo juzi kwenye mazishi ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Jitegemee, Mji mdogo wa Mirerani, Leah Mkwizu Maduhu.

Alisema Mwalimu Leah alikuwa kiongozi mahiri wa Shule ya Jitegemee na ameacha alama kwa kuwa shule hiyo ipo kwenye nafasi nzuri kwenye taaluma kwa sababu kiwango cha ufaulu wa darasa la saba ni asilimia 90 hadi 95.

Alisema Mwalimu Leah alikuwa msimamizi mahiri na aliwahi kuwapa Sh. milioni 13 walimu wa shule sita kila mmoja ili wajenge madarasa, ambapo marehemu alifanya ziada kwa kuanza msingi wa darasa lingine.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania, (CWT), wilayani Simanjiro, Abraham Kisimbi, alisema wamepata pigo kwa kuwa marehemu alikuwa ni mtu wa kujitoa kwa wengine.

Mwalimu Kisimbi alisema umati wa watu uliojitokeza kwenye mazishi ya marehemu Mwalimu Leah umedhihirisha kuwa watumishi na jamii kwa ujumla ilikuwa inamtegemea kwa ushirikiano.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Endiamtu, Mwalimu Regina Anney, alisema watamkumbuka Mwalimu Leah kwa mambo mengi ikiwamo ucheshi na kusaidia wengine. Anney alisema walimu wa eneo hilo wanapaswa kushirikiana na kuonyesha umoja na upendo kila wakati ili kumuenzi marehemu.

Karani wa Kanisa la Waadventista Wasabato, Mirerani Central, Richard Japhet, akisoma wasifu wa marehemu alisema alizaliwa jijini Arusha, Agosti 8, mwaka 1973.

Alisema Mwalimu Leah alisomea ualimu Chuo cha Kinampanda Singida na Marangu mkoani Kilimanjaro na alianza kufundisha Shule ya Msingi Mirerani, mwaka 1996 na akahamia Shule ya Msingi Jitegemee mwaka 2004.

Alisema marehemu alikuwa anasumbuliwa na kisukari na kusababisha figo kushindwa kufanya kazi, vidonda vya tumbo na lehemu.

Aliongeza kuwa marehemu alifariki dunia katika Hospitali ya Muhimbili jijini Dar es Salaam, akiwa na umri wa miaka 47 na kuacha mume, watoto wawili na mjukuu mmoja.

# Kada wa CCM ashauri makatibu wa matawi walipwe mishahara

**Na Paul William,** SAME

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, amekishauri chama kuanza kuwalipa mishahara makatibu wa matawi wa chama hicho, ili waweze kufanya jukumu la kukusanya ada ya wanachama kwa ufanisi na pindi wanaposhindwa kutekeleza wawajibishwe.

Boisafi alitoa kauli hiyo jana, wakati wa kumpokea Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake (UWT), Jesca Mbogo, ambaye ameanza ziara ya siku tatu mkoani Kilimanjaro.

Alisema makatibu hao wamekuwa wakisuasua katika zoezi la ukusanyaji wa ada za wanachama kutokana na chama kutowathamini kwa kulipa mishahara au posho za mwezi zinazoendana na kazi wanayoifanya.

"Ulipaji wa ada za wanachama katika Mkoa wa Kilimanjaro umekuwa ukisuasua na hii inatokana na wanaokusanya ada hizo kutowajibika ipasavyo na hii ni kutokana na kuona jinsi chama kisivyowajali kwa kuwalipa posho wala mishahara ya mwezi, hivyo nikuombe wewe mtendaji ulichukue hili suala na kulifikisha katika vikao vyenu ili lipatiwe ufumbuzi," alisema Boisafi.

Mwenyekiti huyo alisema chama hicho kinapaswa kujipambanua na kuona watu hao hawawezi kufanya kazi iliyotukuka kama wataendelea kufanya bure kwa kuwa kwa sasa hakuna kazi ya bure. Akizungumzia suala la bima za afya, mwenyekiti huyo alisema kuwa, suala la bima kwa sasa ni tatizo kubwa na kuiomba serikali kuingilia sakata hilo ili kuweza kulitafutia ufumbuzi.

Alisema kuwa, viko vikundi ambavyo vilikuwa vimejisajili katika Bima ya Afya ya Taifa, ili kuwawezesha wanachama wake kupata huduma ya afya kwa gharama nafuu, lakini katika hali ya kushangaza vikundi hivyo vimefutwa.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu huyo wa UWT Taifa, Jesca Mbogo, alisema lengo la ziara yake ni kufufua uhai wa chama ili kuhakikisha kinafanya vizuri katika uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu.

Jesca alitumia pia nafasi hiyo kukipongeza CCM Mkoa wa Kilimanjaro kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha chama hicho kinashinda marudio ya uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata 19 na ule wa Jimbo la Siha.

Alisema wana CCM wakishirikiana kwa pamoja na kuweka nguvu moja bila kuruhusu makundi ndani ya chama hawatawapa nafasi wapinzani kupita katikati yao na kuiba mbinu na mikakati ya ushindi pindi wanapoingia katika uchaguzi mbalimbali wa serikali.



Diwani wa Kata ya Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, akishiriki zoezi la ugawaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika kata yake. **PICHA: JAMES LANKA**

# Jela miaka 30 kwa shambulio la ngono

**Na Mary Mosha,** HAI

SHAMBULIO la ngono dhidi ya mwanafunzi mwenye umri wa miaka tisa, limempeleka jela miaka 30, Elihuruma Mushi, ambaye ni mkazi wa kijiji cha Sanya Station Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Baada ya kitendo hicho, pia mshtakiwa huyo alitekeleza shambulio lingine la kingono kwa kumvua nguo mtoto mwingine wa kike mwenye umri wa miaka minne na kumshikashika sehemu zake za siri.

Katika hukumu iliyosomwa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Hai, Devotha Msofe, mshtakiwa amehukumiwa kutumikia kifungo hicho kutokana na vitendo alivyovifanya kuwa ni vibaya na ambavyo havipaswi kufumbiwa macho katika jamii.

Wakati anasoma hukumu hiyo, hakimu huyo alidai kuwa mahakama hiyo imejiridhisha pasipo shaka kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo, huku akijua ni kosa kisheria.

Hakimu Msofe alisema adhabu hiyo itakuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia za kunyanyasa watoto kingono.

Katika kesi hiyo, mahakama ilisikiliza ushahidi uliotolewa na mashahidi sita wa upande wa mashtaka akiwamo mwathirika mwenyewe wa tukio hilo, shahidi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Wilaya ya Hai na daktari wa wilaya hiyo, aliyefanya uchunguzi dhidi ya mwathirika wa shambulio hilo la kingono.

Kosa hilo ni kinyume na kifungu 130 (1) (2) (e) na kifungu 131 (1) kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na mwendesha mashtaka Lobulu Mbise, kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 6, mwaka 2017, saa 7:30 mchana, katika Kijiji cha Sanya Station na kisha kutoroka, lakini alikamatwa baadaye.

Hati ya mashtaka katika kesi hiyo inaonyesha kuwa watoto hao waliofanyiwa shambulio hilo la ngono, wanaishi na bibi yao.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mwendesha mashtaka aliomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa hasa kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo.

# Dk. Mghwira ataka wajane wasaidiwe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amewataka viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasaidia wanawake wajane ili waweze kupata haki zao.

Akizungunza na Nipashe ofisini kwake alisema, katika Mkoa wa Kilimanjaro wajane wengi wamekuwa wakinyanyaswa kwa kudhulumiwa mali baada ya waume zao kufariki hali inayosababisha migogoro katika familia.

Alisema wajane wengi wanapoteza haki zao baada ya waume zao kufariki, hali ambayo inasababisha kubaki na visasi, huzuni na ongezeko la watoto wa mitaani na magonjwa kutokana na msongo wa mawazo.

"Nawaagiza viongozi wote kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasimamia na kutetea haki za wajane baada ya wenzi wao kufariki, ili kupunguza migogoro na dhuluma kwa wajane na watoto," alisema mkuu wa mkoa.

Alisema umefika wakati kinamama kuwa na sauti moja ya kukemea ukatili, ukeketaji na kurithiwa baada ya waume zao kufariki, hali ambayo inaleta ongezeko la mitafaruku katika familia na kukwamisha maendeleo.

Alisema viongozi wote hasa wa wilaya na mkoa wahakikishe wanafanya kazi ya kuwa wasuluhishi wa migogoro katika kutoa elimu kwa wananchi ili kuondokana na mila na desturi za ukandamizaji wa wanawake katika jamii.

"Nawaomba viongozi wa dini kuombea amani, kuwapa wananchi wa mkoa matumaini mapya kwa kuwapa ushauri, nasaha za kuachana na vinyongo vilivyosababishwa na kudhulumu mali kwa muda mrefu ... kwa kuwa na vinyongo, hasira na mambo yanayofanana na hayo husababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo kansa," alisema.

Baadhi ya wajane katika Wilaya ya Moshi, Faustina Msaki, alikiri kuwapo kwa ukatili kwa wajane baada ya wenzi wao kufariki na kuiomba serikali kukemea jambo hilo kwa vitendo bila kupokea rushwa kwa wenye nacho.

"Tunaiomba serikali, mbali na kushiriki kwenye vikao vya familia na kutoa elimu, pia mahakama zetu zisimamie sheria, haki na usawa bila kumtizama mwenye nacho," alisema Elisaria Masawe(61).

# ama

ALHAMISI JANUARI 24, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

## Viungo sita vya mwanadamu vilivyopoteza umuhimu wake



Ukurasa 15

## Mwanamume anavyoshikilia tiba kichaa cha mimba



Ukurasa 14

## Vijana katika hatari zaidi ya pumu




## RC SHINYANGA:

# Kila mwaka tunazika darasa na nusu wazazi, shule nzima watoto

Ukurasa 19

## Vijana katika hatari zaidi ya pumu

**London, Uingereza**

UTAFITI wa Chama cha Watu Wenye Pumu nchini Uingereza, kimetahadharisha kwamba vijana ni kundi katika jamii lililo hatarini zaidi kuugua pumu, kuliko makundi mengine yote.

Katika kundi la watu waliohojiwa na kugundulika, wagonjwa wa pumu ni zaidi ya mara mbili ya wazee na imegundulika wengi walianza kuugua utotoni, lakini walipuuzia.

Inaelezwa kwamba, kuna mikasa mingi watu wanaaanza na kupuuza utotoni, lakini wanajikuta katika hatua mbaya wanapokuwa vijana wakubwa.

Amy Pay, ni kijana mwenye miaka 27, anaeleza mkasa wake akisema: " Watu haiwaingii mawazoni kwamba pumu inaua, hadi wanaopofikia katika ujana. Sikuichukulia pumu kwa uzito mkubwa.

Anasema, alianza kushuhudia mtihani mkubwa pale alipoingia katika mitihani ya kuamka usiku, kukohoa sana kupumua kila mara, ndio ilimpa shida

Mtaalamu wa pumu, Dk. Samantha Walker, anaeleza cha muhimu ni hatua kuchukuliwa kusimamia kanuni na miongozo ya tiba. **BBC**



Mgonjwa wa pumu, aliyeeleza mkasa wake. **PICHA: BBC.**

AFYA

# Waziri Ummy ajinasibu, sekta ya afya nchini inaelekea pazuri



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

UWEKEZAJI wa serikali unaelezwa kuwa bado unaendelea katika sekta ya afya na hali hiyo imechangia sekta kukua kwa kasi, huku ikisaidia kuboresha huduma za afya, ikiwamo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Ni mambo ambayo yamefanya kuendelea kupatikana huduma bora na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema sekta ya afya nchini inaendelea kukua kwa kasi na inaboreshwa.

Katika maboresho hayo, vinavyoendelezwa ni pamoja na dawa, vifaa na vifaa tiba, huduma za chanjo, huduma za afya ya uzazi na huduma za dharura.

Waziri Ummy anasema katika mwaka 2018, jumla ya wajawazito 2,086, 930 walihudhuria na kuandikishwa kuhudhuria kliniki, ikilinganishwa na wajawazito 2,009,879 wa mwaka 2017.

> **Mjamzito anapohudhuria kliniki kwa wakati anafanikiwa kujifungua salama.**

Mwongozo wa utoaji huduma za afya ya uzazi na mtoto, unaelekeza wajawazito kuanza huduma mapema kabla ya majuma 12 ya ujauzito na kuhudhuria kliniki, angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito.

"Mjamzito anapohudhuria kliniki kwa wakati anafanikiwa kujifungua salama," anasema Waziri Ummy.

Anaeleza kwamba, katika mwaka 2018, jumla ya watoto 1,568,832 walizaliwa, ikilinganishwa na 1,498,488 wa mwaka 2017.

Anasema, mahali hapo walipatiwa huduma mbalimbali za chanjo kuzuia magonjwa yanayowaathiri watoto, ikiwamo ugonjwa wa kupooza, kuharisha, pepopunda, homa ya mapafu, homa ya ini na surua.

"Katika kipindi cha mwaka 2018, hali ya chanjo kwa watoto nchini imeendelea kuwa katika kiwango cha juu zaidi ya asilimia 85 ya kiwango kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kama inavyoonyesha chini" anasema.

Waziri Ummy anasema, mwaka 2018 kumetokea vifo 20,087 ikilinganishwa na 19,693 vya mwaka 2017.

Katika kipindi hicho cha miaka miwili; homa ya mapafu iliongoza kuchangia vifo duniani, rekodi ikionyesha mwaka 2017 ilichangia asilimia 18.2 ya vifo na mwaka 2018 asilimia 12.9.

Waziri Ummy, anaendelea kusema mwaka 2018, ugonjwa usio wa kuambukiza wa shinikizo la damu, umejitokeza katika magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha vifo, ikibeba asilimia 1.9 ya vifo vyote.

Waziri Ummy anasema, hali ya upatikanaji dawa muhimu katika vituo vya kutoa huduma za afya nchini, imeendelea kuimarika na serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka Sh. milioni 31 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia Sh.milioni 251 mwaka 2016/17 na kuvuka kuelekea Sh. milioni 270 katika mwaka uliopo wa fedha.

Waziri Ummy anasema kuwa, hali ya upatikanaji wa damu salama katika kipindi cha mwaka 2018 imeongezeka, huku jumla ya chupa za damu salama 307,835 ambazo ni sawa na asilimia 85.5 ya lengo zilikusanywa, ikilinganishwa na chupa 233,933 mwaka 2017.

Pia, anawashauri wananchi waendelee kujitokeza kuchangia damu, ili kuendelea kuokoa maisha ya wahitaji. Waziri Ummy anasimulia: "Chupa zote 307,835 zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu, pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni Ukimwi (HIV,) Homa ya Ini B na C (HBV, HCV) na Kaswende."

"Jumla ya chupa 262,283 sawa na asilimia 85.3 zilikuwa salama na kusambazwa katika hospitali kwa ajili ya wagonjwa wenye uhitaji wa damu," anasema Waziri Ummy.

Waziri Ummy anasema kwamba, katika mwaka 2018 jumla watu 47,967 waligundulika kuwa na vijidudu vya kifua kikuu, ikilinganishwa na wagonjwa 44,714 waliogunduliwa mwaka 2017, huku akisisitiza tatizo la ugonjwa wa kifua kikuu imeendelea kuwapo takribani mikoa yote nchini.

Waziri anasema, hadi kufikia Desemba mwaka jana, jumla ya vituo vya kutoa huduma za afya vimefikia 7,768 kutoka 7,435 mwaka 2017 sawa na ongezeko la vituo 333 kwa mwaka.

Anadai, serikali ilikuwa inamiliki asilimia 71 ya vituo vya kutoa huduma ambavyo ni: Mashirika ya dini asilimia 12; taasisi za serikali asilimia tatu; na vituo binafsi asilimia 15.

Katika hatua hiyo Waziri Ummy anasema kwamba, hadi kufikia Desemba mwaka jana, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulikuwa na wanachama 899,654 ikihudumia jumla ya wanufaika 4,219,192 sawa na asilimia nane ya Watanzania wote.

AFYA

# Mwanamume anavyoshikilia tiba ya kichaa cha mimba

**Na Renatha Msungu**

***"...Dk. Mdachi anataja silaha yao kuu ni kuwafariji kinamama hadi wafikie hatua ya kusahau maumivu wanayopata wakati wa kujifungua."***



Mama mjamzito.



NI vigumu kuaminika, lakini ndivyo ilivyo katika ugonjwa wa kichaa cha mimba unaowaangukia kinamama wajawazito. Sababu kubwa inayochangia katika hilo, ni mama mjamzito kupatwa na maumivu makali, hususani wakati wa kukaribia kujifungua.

Maumivu hayo ni makali sana na hayazuiliki kwa mwanamke. Hapo ndipo anaelezwa anahitaji upendo wa hali ya juu kutoka kwa mume, mpenzi au mtu mwingine mwenye ukaribu naye, akiwa ndiye tiba kubwa inayoangukia katika saikolojia kwa mama huyo wakati wa hali hiyo ngumu.

Tabibu anayejitambulisha kwa jina la Dk. Mdachi, kutoka Hospitali ya Rufani Amana, jijini Dar es Salaam, anasema inapotokea mjamzito amekumbwa na hiyo, hakuna tiba mbadala ya maradhi ya akili, akirejea mfano wa huduma inayotolewa katika Hospitali ya Akili ya Mirembe, mkoani Dodoma.

**INATOKOMEZWAJE?**

Ni swali ambalo Dk. Mdachi analielekeza kwa kinababa, kwamba wana mchango katika uzazi huo. Katika mazingira hayo, wajibu wao mkuu ni kuwa karibu na wake zao kuanzia kipindi cha ujauzito mpaka wanapojifungua.

Katika hilo, Dk. Mdachi anataja silaha yao kuu ni kuwafariji kinamama hata wanafikia hatua ya kusahau maumivu wanayopata wakati wa kujifungua.

Imani ya kitaalamu kutoka kwa daktari huyo ni kwamba, iwapo wanaume wengi watajituma kwa namna hiyo dhidi ya wake au wenza wao wanapokuwa katika ujauzito, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza maradhi ya kichaa cha mimba.

Anasema ni maradhi hatari, kwani sababu kuu anayoitaja ni kwamba wako katika hatari ya kupata kutokana na ukweli kwamba, ni maumivu yasiyokwepeka.

Dk. Mdachi anarejea mtazamo wa kihistoria kwamba ni maradhi ambayo yapo kwa kipindi kirefu na imeshawadhuru wengi kiafya, hali inayoendelea hadi sasa.

Kwa mujibu wa Dk. Mdachi, ni hali inayotokea ndani ya muda mfupi, lakini una madhara mabaya, hata ya mzazi dhidi ya mwanawe baada ya kujifungua.

"Kwa sababu, huwezi kumuachia kichaa alee mtoto hapo. Katika hali ya kawaida, atakuwa katika mazingira hatarishi kipindi kichaa chake kitakapopanda na kuanza kukurupuka kwa kila analofanya," anaeleza mtaalamu huyo.

...Dk. Mdachi anataja silaha yao kuu ni kuwafariji kinamama hadi wafikie hatua ya kusahau maumivu wanayopata wakati wa kujifungua.

Anachosistiza ni wake kwa waume kuwa kitu kimoja katika kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mimba, wakipata elimu kutoka jamii ya Kitanzania.

Daktari huyo anasimulia maumivu ya mwanamke wakati wa kujifungua kwamba ni makali katika kiwango kilichopitiliza, unamtia wazimu mara tu anapojifungua. Anasema, ni matukio yanayojitokeza kila mara katika hospitali nyingi, tiba ya dharura ikiangukia katika dhana ya upendo kwa wanawake.

Kwa mujibu Dk. Mdachi, mbinu sahihi imesimama katika kuwakanya na kutokasirishwa na mambo madogo yanayoweza kuwapatia madhara kama hayo ya kisaikilojia.

Anasema kuna kampeni kubwa inayofanyika katika kukabili kichaa cha mimba, lakini inakwazwa na uhalisia kwamba, dawa yake ambayo ni upendo inaangukia katika saikolojia ya watu wawili wanapoishi pamoja.

"Huwezi kuzuia mtu asibebe mimba, kisa kuogopa kupata kichaa. Ni lazima azae, maadamu na yeye alizaliwa kama Biblia inavyosema, zaeni mkaijaze dunia," anasema Dk. Mdachi.

**WANAWAKE JE?**

Rai kuu ya kinamama wanaielekezea kwa serikali kuunda kanuni na sheria zinazotoa adhabu kali kwa kinababa wanaosababisha maradhi hayo kwa wanawake.

Aisha Mohamed, ni mwanamama mwenye maoni yanayoendana na mtazamo wa Dk. Mdachi, anasema kwamba upendo ni jambo muhimu zaidi kwa mke, anapokuwa katika ujauzito.

Dai la Aisha ni kwamba, katika familia nyingi kuna wanaume wengi ambao wake zao wanapokuwa katika ujauzito, wanatumia vyema fursa hizo kutoka na marafiki zao kushinda katika starehe za nje kama vile ulevu, pasipo kujali wajibu wao wa msingi kwa familia zao katika wakati huo.

Anafafanua kwamba, tabia hiyo inapaswa kupigwa vita na madawati ya kijinsia katika taasisi mbalimbali zinazosimamia haki za binadamu, ili kuwafanya wakinababa waridhie mtazamio wa heshima na uwajibikaji katika ndoa zao.

**KINABABA JE?**

Mtazamo wao ni kwamba, ni vyema elimu hiyo ikatolewa kwa jamii yao wajue chanzo cha adha hiyo ya kiafya kwa kinamama wanapojifungua na hatua inayotakiwa kufanyika, ili kuondoa tatizo hilo kwa jamii kwa ujumla.

Wataalamu wanasema ni vyema wanaume kufikiria kuokoa wake zao katika majanga hayo, kwa sababu ni ugonjwa hatari kwa wanawake na jamii nzima kwa ujumla.

Juma Matheo, anakiri walakini kwamba kinababa wengi hawajui dhana nzima ya kichaa cha mimba na namna kinavyotokea, hivyo inaangukia katika uzembe wao wakikiona ni ugonjwa kama yalivyo mengine.

Anashauri kinachotakiwa kufanyika ni kutolewa elimu ya hatua inayotakiwa kuchukuliwa kwa wake zao kipindi wanapokuwa na ujauzito, ili waweze kuwasaidia.

Msisitizo wake ni kwamba, ni muhimu sana elimu itolewe kila siku ili wanaume wajue wajibu wao katika kuokoa maisha ya kinamama katika kipindi cha ujauzito.

MAZINGIRA

# Shida maji inavyowahenyesha wauguzi, daktari kupangiana zamu kuchota maji

• Familia zaanza alfajiri bondeni, kisha shambani



Wanakijiji cha Mpale, Korogwe katika tukio linalohusu uzunduzi wa mradi wa umeme kijijini, mwaka juzi. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Jenifer Julius,** aliyekuwa Korogwe

REHEMA Athumani ni miongoni mwa wanawake1740 katika kijiji cha Mpale, wilayani Korogwe wanaojivunla kuishi katika eneo lenye maji ya kutosha yanayotiririka kutoka kwenye chemchem za milima inayowazunguka.

Kila siku asubuhi analazimika kuwapo shambani anakolima chai, ambayo ni zao lao kuu la biashara katika kijiji hicho, likifuatiwa na hiliki, mahindi na miwa.

Cha kustaajabisha kutoka katika ratiba ya mama huyo mwenye umri wa miaka 35, huwa analazimika kuamka saa 11.00 alfajiri akianza na kusaka maji, ili awahi kwenda shamba kabla ya jua halijawa kali.

Ni mwendo wa takribani nusu saa unaoandamana na kadhia ya kupanda milima na kushuka mabonde kufika eneo yanakopatikana maji, huku mwenyewe anakiri:"Kwa kweli tuna maji ya kutosha ya chemchem, tatizo lililopo ni kwamba yanapatikana mbali."

Adha ya uhaba wa mabomba ya maji unaokikabili kijiji hicho, sio jambo geni kwa kuwa vijiji vya jirani kama vile Bungu, Kwemanolo, Tewe na Mali navyo vinakabiliwa na shida hiyo.

Mazingira hayo yanatofuatiana na baadhi ya vijiji vilivyopo ndani ya wilaya hiyo, ambavyo licha ya

> **Ingawa sijawahi kusikia taarifa yoyote mbaya, lakini siwezi kumwacha mke wangu aende kuchota maji mwenyewe, kwa sababu kuna mapori wanyama wakali waweza kuvamia.**



Kinamama wa kijiji cha Mpale, wakichota maji. **PICHA: JENIFER JULIUS.**

kuwa mbali na vyanzo vya maji ,vina mabomba yanayosambaza maji safi na salama.

Kijiji cha Kwasemangube, kilichokuwa umbali wa kilomita 45 kutoka Mpale ni moja ya mifano hai kuwa kumtua mwanamke ndoo inawezekana.

Wanawake wa kijiji hicho wanafurahia kuondokana na kadhia hiy, iliyodumu kwa muda mrefu.

Mwanamama Flora Shemweta, anajivunia kuwa, hawana changamoto ya mabomba ya maji kijijini hapo, kwa kuwa katika wastani wa kila kaya 10, mbili zina mabomba ya maji. Hiyo ni sawa na asilimia 20 ya watumiaji wote wa maji.

"Ingawa mabomba sio mengi lakini tunashukuru hatutembei umbali mrefu kusaka maji," anasema flora.

Rehema anasema, anatumia kati ya saa mbili na tatu kuchota maji, hali inayomchosha na kuna wakati anashindwa kabisa kwenda shamba.

Mama huyo anasema, kila anapomaliza kuchota maji, ndipo anapopata maumivu ya kichwa na miguu, kutokana na kubeba ndoo kwa muda mrefu, ikiendana na safari ya kupandisha na kushusha milima.

Mwingine katika kundi hilo la wenye simulizi ni Zaharia Malik, anayesema wanalazimika kununua maji kwa kila dumu Sh. 500, ili kuongezea kidogo anayochota mumewe, kwani wana mtoto mchanga, hali inayofanya kuwapo mahitaji makubwa ya maji.

"Tunaiomba serikali itujengee mabomba karibu na makazi ili kutupunguzia mzigo huu," anasema Zaharia.

Inaelezwa ni tatizo lisiloishia kuathiri wanawake pekee yao, bali inaenda mbali hata kwa wanaume ambao baadhi yao wanalazimika kuchelewa kwenda kwenye shughuli zao za maendeleo, ili kuwasaidia wake zao.

Jafari Muhidini, ni mwanamume anayechukulia uzoefu binfasi kwamba, hulazimika kuchelewa kwenda shamba asubuhi, akianza na jukumu la kuamka mapema kumsindikiza mke wake kuchota maji, kusimamia usalama wake, akihofia jambo baya linaweza kumpata.

"Kama maji yangekuwa yanatoka bombani eneo la karibu, ningekuwa natangulia shamba kisha mke wangu anakuja akishamaliza kazi zake," anasema jafari.

Anaongezea kuwa, kutokana na uhalisia huo, analazimika kutoa kipaumbele cha ulinzi wa mkewe wakati wa kuchota maji, ya matumizi ya majumbani mwao.

"Ingawa sijawahi kusikia taarifa yoyote mbaya, lakini siwezi kumwacha mke wangu aende kuchota maji mwenyewe, kwa sababu kuna mapori wanyama wakali wanaweza kuvamia," anasema Jafari.

### ZAHANATI MPALE

Zahanati ya Mpale, ni moja ya vyombo muhimu cha kutoa huduma ya kijamii katika eneo hilo, ambayo imeathirikwa na kutokuwapo huduma ya maji karibu.

Chombo hicho cha kusimamia afya ya wananchi, inahudumiwa na wauguzi wawili na daktari mmoja, wanaopeana zamu ya kuchota maji ya kuendeshea shughuli za kitabibu, kabla ya kuanza kuhudumia wagonjwa

Eunice Mpurua, muuguzi katika zahanati hiyo, anasema kutokuwapo huduma ya maji karibu na zahanati hiyo, kunachelewesha huduma kwa wagonjwa.

"Huwa tunapeana zamu, wakati nesi mmoja akihudumia wagonjwa, mwingine anakwenda kuchota maji na kufanya usafi "anasema Eunice.

Anasema ni hali inayosababisha wagonjwa kukaa foleni muda mrefu akisubiri huduma, jambo ambalo lisingetokea iwapo kungekuwapo usaidizi wa kikazi.

Eunice ana mtazamo kwamba kuwapo mabomba ya maji katika zahanati hiyo, licha ya kurahisisha utoaji huduma, pia kutawasaidia wanakijiji kupata maji safi na salama, kwa kuwa yatachujwa na kuwekwa dawa.

Anaongeza kuwa, maji yanayotiririka wakati mwingine yanakuwa si salama, kwa kuwa huambatana na uchafu kama vile vinyesi vya wanyama na binadamu.

### MWENYEKITI KIJIJI

Augustine Mganga, ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpale, anakiri kuwa shida maji imeshamiri katika kijiji hicho na wanawake ndio waathirika wakuu.



Wanakijiji wa Magundi, tarafa ya Bungu wilayani Korogwe, wakichota maji katika mazingira duni. **PICHA: BLOGU TANGA HURU.**

> **Natamani serikali itumie mtambo wa umemejua wa Ensol, ili watuchimbie visima na kutuwekea mabomba ya kupampu maji.**

Anaeleza hamasa yake katika kutamani kampeni ya 'kumtua ndoo mwanamke,' ifike kijijini hapo kwa kuwa wanawake hao wameteseka kwa muda mrefu.

Mganga anasema, mamlaka za kiserikali ilifika mahali hapo mwaka juzi na kupima ramani, hivyo wanasubiri kufungiwa mabomba.

Anaeleza zaidi kwamba, kwa sasa wana mtambo mkubwa wa umemejua kijijini hapo, serikali inaweza kuutumia kupandisha maji na kuyahifadhi kwenye matanki makubwa na kuweka mabomba ambayo wanakijiji watachota maji kwa gharama ndogo.

"Natamani serikali itumie mtambo wa umemejua wa Ensol, ili watuchimbie visima na kutuwekea mabomba ya kupampu maji," anasema.

Takwimu za Huduma ya Maji kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, zinaonyesha katika mwaka wa fedha 2015/2016, hali ya usambazaji maji katika wilaya ya Korogwe ilikuwa kwa wakazi 52,611 ambao ni sawa na asilimia 72 , Huku mkoa wa Tanga ukiwa katika mikoa 5 inayoongoza kutoa huduma ya kusambaza maji.

## Dk. Ndugulile: Asilimia 52 ndio wanapima VVU

• Upimaji mpya sasa unaanzia miaka 15

**Na Yasmine Protace**



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile. **PICHA: MTANDAO**

UPIMAJI wa afya ni njia mojawapo na muhimu inayomsaidia mtu kufahamu kinahomsumbua au uhalisia wake mwilini na kukifanyia kazi.

Kupitia kauli na wito wa wataalamu wa afya, imekuwa ikihamasishwa kila mara watu wapime afya zao, katika lengo la kuwasaidia kujitambua na kuweza kuanza njia za kupata matibabu.

Inaelezwa kwamba, iwapo mtu hatakuwa tayari kupima afya yake na akajua kinachomsumbua anaweza kujipanga kimaisha na kujikubali mwenyewe, huku akiendelea na harakati za matibabu.

Kama mtu hatakuwa tayari kupima afya yake ataendelea kuishi maisha ya wasiwasi kila siku. Hilo ndilo linaloifanya serikali iendelee kuhamasisha jamii kupima afya zao kwa faida yao.

Uhamasishaji umekuwapo, kuna kampeni mbalimbali za kuelimisha jinsi jamii inavyoweza kuepukà maradhi na imesema kuna Watanzania 2,405,296 hadi Oktoba mwaka jana, waliopima afya zao dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anasema inafanyika kupitia kampeni iitwayo 'Furaha Yangu' na wanaopima ni asilimia 52 ya lengo la kuwapima Watanzania 4,638,639, ikidhamiriwa hadi Desemba iliyopita.

Dk. Ndugulile, aliiambia Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii jijini Dodoma na anafafanua: "Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2018 jumla ya Watanzania 2,405,296 walikuwa wamepima VVU (Virusi vya Ukimwi) kupitia kampeni ya 'Furaha Yangu' ambao ni sawa na asilimia 52 ya lengo la kuwapima Watanzania wapatao 4,638,639 hadi Desemba 2018."

Naibu Waziri anasema katika mchanganuo waliopima, wanaume wako asilimia 44 na wanawake asilimia 56 na katika jumla yao wote watu 70,436 ambao ndio asilimia 2.9 walikutwa wameambukizwa, mgawanyo ulioko; wanaume 27,984 na wanawake 42,452.

Anasema, wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ukimwi namba 28 ya mwaka 2008, ili kupendekeza marekebisho yatayoruhusu upimaji binafsi wa VVU.

Dk. Ndugulile anasema kuwa serikali ipo katika mchakato wa kupunguza umri wa kupima VVU kwa ridhaa ya mzazi au mlezi kutoka miaka 18 hadi 15, kutokana na kasi ya maambukizi kuongezeka katika umri huo.

Anasema, wizara imeendelea kutoa huduma za tohara ya kitabibu kwa wanaume, lengo ni kuzuia kuenea VVU kutoka kwa mwanamke kwenda kwa mwanaume katika mikoa ya kipaumbele isiyo na utamaduni wa tohari na ina kiwango kikubwa cha VVU.

"Hadi kufikia Septemba, 2018 mikoa 17 inatoa huduma za tohara, ambayo ni Iringa, Njombe, Tabora, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera, Singida, Kigoma, Mara na Morogoro," anasema Dk. Ndugulile

Pia, anasema serikali inaendelea kuhudumia tohara kwa wanaume, bila ya malipo katika vituo vya huduma za afya na hadi kufikia Septemba 2018, jumla ya watu 3,702,387 wamefanyiwa tohara nchini.

Dk. Ndugulile anasema, hadi kufikia Desemba mwaka jana, wizara iliandikisha katika huduma za tiba na matunzo watu wanaoishi na VVU wapatao 1, 087,382.

"Watu 68,927 waliandikishwa katika kipindi cha robo ya mwaka cha Julai hadi Septemba 2018 ambapo kati yao 1,068,282 wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU, ambao watoto walikuwa 58, 908," anasema.

AFYA

# Viungo sita vya mwanadamu vilivyopoteza umuhimu wake



Sikio. Kando ni wanyama wanaohusishwa. **PICHA ZOTE: BBC**

MABADILIKO ya kidunia hivi sasa yanachukua nafasi, katika maumbile ya mwili wa mwanadamu na mwanahistoria wa binadamu Dorsa Amir, katika chapisho lake la mtandao wa Twitter, anasema:"Mwili wako kimsingi, ni makumbusho ya historia ya asili."

Katika mabadiliko yaliyoko, inaelezwa kuna viungo sita vya binadamu vilivyoachwa katika matumizi ya mazoea:

1. Misuli iliyopo chini ya kiganja cha mkono; Misuli iliyopo chini ya kiganja cha mkono, ilitumika kumsaidia binadamu kupanda juu ya miti.

Mfano mmojwapo, ni kwamba kuwekwa mkono katika eneo lilolo tambarare kama meza, halafu mtu aguse kidole kidogo hadi kikubwa cha mkono wake.

Je unaona misuli karibu na kiganja chako cha mkono? Hiyo ndio inayoitwa Palmaris longus.

Inalaezwa kitaalamu, takriban asilimia 18 ya watu duniani hawana misuli hiyo na kutokuwepo kwake, hakushirikishwi na mapungufu yoyote ya kimwili.

Misuli hiyo inapatikana kwa sokwe wanaopendelea kupanda miti. Hapo, ikimaanisha kwamba, ilikuwa ikitumika kusaidia kupanda miti.

Siku za karibuni, misuli hiyo inapendelewa sana na madaktari wa upasuaji na Dorsa anatamka: "Huitumia mara kwa mara katika upasuaji kwa kuwa haitumiki sana katika kazi za mkono.'

2. Uvimbe mdogo katika sikio; Mwandishi wa vitabu, Jerry Coyne anatamka:"Iwapo unaweza kuchezesha sikio lako basi unaonyesha mabadiliko ya binadamu.'

**Wakati tulipoanza kupoteza baadhi ya nywele hizo mwilini, msisimko huo ulianza kukosa maana hadi kufikia kiwango cha kukosa kazi ya kufanya.**



Kigubiko cha jicho.



Kiungo cha mwili, mithili ya mkia wa mtu.

Uvimbe mdogo uliopo juu ya sikio ni mojawapo ya misuli hiyo.

Miongoni mwa wengi, misuli hiyo haina maana yoyote, lakini wanaweza kuitumia kuchezesha masikio yao.

Kimsingi, mjadala wa kuwapo msuli ulikuwa mkubwa na inadaiwa kuwa msuli huo wa sikioni unaonyesha mabadiliko.

Misuli inatumika katika muundo wa mwili wa paka na farasi, wanaochezesha masikio yao kama inavyoelezwa na Coyne.

Hiyo inawasaidia kukabiliana na wanyama wengine, kuwatafuta watoto wao na kuelewa sauti nyingine.

3. Mfupa wa mkia; Dorsa Amir, anasema kwamba mfupa wa mkia nao ni mabaki ya mabadiliko katika binadamu na kwamba tulikuwa na mikia iliyotumika kusawazisha mwendo wao katika miti.

Kiungo hicho ni mojawapo ya mifano mizuri ya viungo vinavyofanya kazi nyingine, kinyume na ilivyokuwa awali.

4. Kigubiko cha jicho la tatu

Je unaiona sehemu ya rangi ya waridi iliopo katika kona ya jicho lako? Hiyo inalaezwa ni mabaki ya kile kinachojulikana, kama utando au 'kigubiko cha tatu' kutokana na mabadiliko ya mwanadamu.

Kigubiko cha jicho la tatu, husonga kutoka kushoto kwenda kulia na kwa sasa wataalamu wanaieleza huduma yoyote katika maisha ya sasa.

Hivyo, vinaonekana katika makundi ya wanyama kama vile ndege na paka.

5. Msisimko wa mwili usiotarajia; Je unajua kitendo anachofanya paka wakati anapohatarishiwa maisha yake?

Ni sawa na vile tunavyopata msisimko wa mwili wakati unaposikia baridi au hata kuogopa kitu. Wanasayansi wanakiita kitendo hicho 'piloerection reflex.'

Dorsa anasema, kutokana na vile tunatumia muda wetu mrefu duniani kama wanyama wenye manyoya, msisimko huo ulikuwa ni mojawapo ya njia za zamani za kukufanya uwe mkubwa zaidi ya ulivyo ama hata kulinda joto kutoka mwilini, wakati anapohisi baridi.

"Wakati tulipoanza kupoteza baadhi ya nywele hizo mwilini, msisimko huo ulianza kukosa maana hadi kufikia kiwango cha kukosa kazi ya kufanya," anasema Dorsa.

6. Mshikamano wa mikono;. Mshikamano wa mkono unaonekana wakati mtoto anaposhikilia kidole kwa nguvu. Kitendo hiki, hufanyika miongoni mwa wanyama wengine.

Dorsa anasema, watoto wanaozaliwa wanakuwa na utayari wa kuwashika wazazi wao, ili kupata mshikamano wa kubebwa.

Lakini, watoto wetu hubebwa wakiwa hawajakomaa vya kutosha, ikilinganishwa na watoto wa wanyama wengine, ambao hawawezi kuinua vichwa vyao na kutembea.

Hizi ni tabia nyingine zinazotokana na mabadiliko ya mwanadamu. lakini ni mabadiliko yasiyomsaidia mwanadamu wa sasa. **BBC.**

AFYA

## RC SHINYANGA:

# Kila mwaka tunazika darasa na nusu wazazi, shule nzima watoto

- Ving'ang'anizi mila, wawekewa mtego
- Mwenyekiti afafanua ubishi ulivyo
- DC asimulia janga la uzazi wake

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

HADI sasa vifo vitokanavyo na uzazi, bado vimeendelea kuwa changamoto nchini, hali ambayo serikali imeamua kulitilia mkazo, kwa kuzindua kampeni inayosaidia kumaliza vifo hivyo.

Kimsingi, ni mada amabayo sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya (MMAM), ambao hadi sasa una wastani wa muongo mmoja tangu uanze kutumika.

Novembe 6 mwaka jana, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, alizundua kampeni inayoitwa 'Jiongeze Tuwavushe Salama' iliyolenga kuongeza uwajibikaji katika kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi nchini.

Mara baada ya uzinduzi huo, kila mkoa uliagizwa kuitekeleza kampeni hiyo, pamoja na kupanga mikakati itakayosaidia ama kupunguza au kumaliza kabisa vifo vitokanvyo na uzazi wa kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Mkoa wa Shinyanga ulizinduliwa kampeni hiyo Januari 18 mwaka huu, kwa kukutanisha wadau wanaoshughulika na afya. Hapo walihusisha asasi za kiraia, lengo ni kuunganisha nguvu na serikali, kupambana na kutokomeza vifo vitokanavyo na uzazi mkoani humo.

**RC SHINYANGA**

Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Zainabu Telack, anakumbusha, bila ya kuuganisha nguvu ya pamoja, tatizo la kutokomeza vifo vya uzazi mkoani humo litakuwa ndoto.

Anasema, kunahitajika mshikamano kati ya mashirika, viongozi wa dini, wazee wa kimila, na watumishi wa serikali kuwa kitu kimoja kwenye mapambano hayo.

Zainabu anadokeza sababu mowajawapo inayochangia kuendelea kuwapo vifo vya uzazi mkoani humo, hasa wajawazito kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati za kujifungulia majumbani, ambako kuna usalama mdogo.

"Changamoto hii ya mila na desturi za wajawazito kupenda kujifungulia majumbani, tusipoweka mkazo wa nguvu na kushikana mashati, kamwe vifo vya uzazi mkoani hapa hatuwezi kuvimaliza," anasema Telack.

"Natoa agizo kwa kila mtendaji wa kijiji mkoani hapa, waanze kuwa na madaftari ya kuandikisha wajawazito kwa kila kaya," anasema na kuongeza:

"Majina hayo yapelekwe pia kwenye huduma za afya za jirani, ili tupate kuwafuatilia wale ambao wanakaidi kuhudhuria kliniki na kujifungulia hospitalini, tupate kuwabana ndipo tutafanikiwa kumaliza vifo vitokanavyo na uzazi."



Wadau wa Afya mkoani Shinyanga, wakiwa kwenye uzinduzi wa kampeni ya uwajibikaji kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

> **Natoa agizo kwa kila mtendaji wa kijiji mkoani hapa, waanze kuwa na madaftari ya kuandikisha wajawazito kwa kila kaya.**



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, akitoa ushuhuda wa alivyonusurika kifo cha uzazi.

Anaeleza mshangao wake, akisema haiwezekani serikali kila wakati inapiga kelele ya kuwataka wajawazito waende kujifungua kunakopatikana huduma za afya, ambako ndiko salama, lakini kunaendelea kuwapo ukaidi na wakifikia hatua mbaya ndipo hukimbilia hospitalini, na hatimaye kufariki na kusababisha vifo vya uzazi kuongezeka.

"Tabia hii ya kuendekeza mila na desturi itakoma tu, na nyea viongozi wa makanisa na wazee wa kimila tuone elimu kwa wananchi labda nyie watawaelewa, waache kuendekeza ma imani ambayo yalishapitwa na wakati, ili tupate kumaliza kabisa vifo vya uzazi Shinyanga na kubakia vile vya mapenzi ya Mungu,"anasema Telack

"Mimi hapa nitaingia mkataba na wakuu wa wilaya na wakuu wa wilaya wataingia na wakurugenzi na wakurugenzi wataingia

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Kila mwaka tunazika darasa na nusu wazazi, shule nzima watoto

INATOKA UK.19

na watendaji kata na vijiji, ili pale kinapotokea kifo cha mzazi, kila mmoja atoe taarifa kwanini kimetokea, hali ambayo itahamasisha uwajibikaji na kumaliza vifo kabisa vya uzazi,"anafafanua.

Mkuu wa Mkoa, anaainisha takwimu za vifo vya uzazi vinavyotokea, akiifananisha na kuzika darasa zima na nusu la wanafunzi, huku kwa upande wa watoto anaiweka sawa na kuzika shule nzima kwa mwaka, hali inayopaswa kupingwa na kila mmoja.

**MGANGA MKUU**

Mganga mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Dk. Rashid Mfaume, anataja takwimu za miaka mitano za vifo vitokanavyo na uzazi mkoani humo, kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka jana, jumla yake ni watoto 4,148 na kimamama 263

Katika mchanganuo huo wa takwimu za Mganga Mkuu, ni kwamba: 2015 vifo vya mama vilikuwa 60; mwaka 2016, walikufa 74; mwaka 2017 walikuwa 73 na mwaka jana, 56.

Dk. Mfaume anataja vifo vya watoto kwa mwaka huo 2015 vilikuwa 1340; (2016) 1080; (2017) 913; na 2018 wako 815, akisema yanahitajika mapambano zaidi ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa mama na watoto wao.

"Sababu za vifo hivyo hutokana na upungufu wa damu kwa wajawazito wakati wa kujifungua, kifafa cha mimba, kupasuka kizazi, matatizo ya moyo, uhaba wa vifaa tiba, upungufu wahuduma wa afya, mimba za ututoni pamoja na kuendekeza mila na desturi za kujifungulia majumbani sehemu ambapo siyo salama," anasema Dk.Mfaume.

Mganga huyo anabainisha mikakati iliyopo, ni kuendelea kutatua changamoto za huduma za afya, ikiwamo kuongeza juhudi za ujenzi wa vituo vya afya na kuongeza hospitali za wilaya.

Anasema, hadi sasa serikali imeshatoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya hospitali ya wilaya ya Shinyanga Vijijini na Ushetu, inayochangia kupunguza vifo vya uzazi.

**USHUHUDA DC**

Nyabaganga Taraba, ni Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, anayetoa ushuhuda namna alivyonusurika kifo wakati wa kujifungua watoto wake, anasema endapo angejifungulia nyumbani, huenda angepoteza maisha.

"Katika uzao wangu wote nilikuwa nikijifungua, watoto wenye uzito wa kilo tano na kama ningeamua kuwa na tabia ya kujifungua nyumbani, huenda labda nisingekuwapo hapa nanyi, kwa sababu nilikuwa katika hali ya hatari,

"Kutokana na kupenda kujifungulia hospitali, maisha yangu yalikuwa salama na leo naishi. Hivyo, napenda tu kutoa wito kwa wanawake wenzangu 'achaneni' na mila ambazo zilishapitwa na wakati za kujifungua majumbani.

"Masuala ya kutumia mizizi siyo wakati wake sasa twendeni kwenye huduma za afya tukapate tiba sahihi," anasema.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, (kulia) akiwa katika tukio la utiaji saini mkataba na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), wa kwenda kufanya kazi ya kumaliza vifo vitokanavyo na uzazi kwenye wilaya yake.

**"Katika Health Centre hizo, mbili hazina wahudumu wa afya ambazo ni Masanga na Sekeididi na tumeshaandika maombi serikalini ili kupata watumishi hao, lakini hakuna utekelezaji.**




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, akizindua kampeni ya uwajibikaji katika kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi 'Jiongeze Tuwavushe Salama' mkoani humo.

**MWENYEKITI KISHAPU**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kishapu, Boniphace Butondo, anasema suala la kutokomeza mila na desturi kwa wajawazito kujifungua majumbani ni mtambuka, licha ya kuwepo zuio la kiserikali na kisheria.

Anachohimiza ni kwamba, serikali inapaswa kujenga karibu huduma za kiafya, zikiwamo vituo vya afya na zahanati.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya unaotekelezwa nchini, kila kijiji kinapaswa kuwa na zahanati na kila kata kuwa na kituo cha afya, hali kadhalika hospitali kwa wilaya na hospitali za mikoa zinakuwa za rufani, juu kukiwapo hospitali za kanda na ngazi ya juu kabisa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Pia, katika taarifa yake ya hivi karibuni, Rais Dk. John Magufuli, alimsifu Waziri wa Nchi katika ofisi yake, anayeshughulika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kuwa wamechukua hatua zinazostahili kuleta mageuzi ya kiutendaji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu - Butondo, analalamika kwamba juhudi za kutoa elimu kwa mjamzito kuacha kujifungulia majumbani, bado hajamuwekea mazingira bora ya kupewa huduma za afya kuwa karibu.

Anaeleza shaka yake kwamba, kuna hatari wajawazito wataendelea kujifungua nyumbani na kusababisha vifo vya uzazi Shinyanga.

"Mfano sisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, kila bajeti ya mwaka wa fedha huwa tunatenga fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za kiafya, zikiwamo ujenzi wa health centre (vituo vya afya) na mpaka sasa tuna vituo hivyo sita, ambavyo vipo katika kata ya Lagana, Ngofila, Sekebugolo, Masanga, Idukilo na Sekeididi," anasema Butondo.

"Katika Health Centre hizo, mbili hazina wahudumu wa afya ambazo ni Masanga na Sekeididi na tumeshaandika maombi serikalini ili kupata watumishi hao, lakini hakuna utekelezaji," anasema.

"Sasa hapo tutamaliza kweli vifo vitokanavyo na uzazi? Lazima tu wajawazito wajifungulie majumbani sababu ya ukosefu wa huduma," anahoji zaidi.

**NGO& WAKAZI**

Mratibu wa Mradi wa Ulinzi wa Mtoto kutoka shirika la Save The Children, Alex Enock, anasema wao kama wadau wanafanya kazi na serikali na anatoa wito kwao katika bajeti ya mwaka wa fedha iliyopo (2019-2020), kipaumbele chao kikubwa kiwe kuajiri watumishi wa afya ili kuondoa upungufu uliopo.

Joyce Sabina ni mkazi wa mjini Shinyanga, anaeleza sababu za kinamama kupenda kuendelea kujifungulia majumbani, kuwa licha ya kuwapo lugha chafu kwa baadhi ya wauguzi, hata umbali wa huduma za afya nazo ni kikwazo na wanajikuta wakihamasika kujifungulia nyumbani kwa msaada wa wakunga wa jadi.

# Wanne wadakwa kwa kuingiza vyandarua kwa njia za panya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wanne wakiwamo raia wawili wa nchi jirani ya Malawi kwa tuhuma za kuingiza shehena ya vyandarua nchini ambavyo havijalipiwa kodi kwa kupitia njia za panya na hivyo kuikosesha serikali mapato.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kituo cha Polisi cha Tukuyu wilayani Rungwe zilipohifadhiwa mali hizo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei alisema watu hao walikamatwa januari 21 majira ya saa 3:15 usiku.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Obley Sambakusi (32) na Tamandani Kachimela (31) wote wakazi wa Lilongwe nchini Malawi, Imtiaz Ahmed (45) na Boazi Salvatory ((28) wote madereva na wakazi wa wilaya ya Kyela mkoani Mbeya.

Kamanda Matei alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwenye kizuizi cha magari kilichopo eneo la Kayuki Kata ya Ilima wilayani Rungwe katika barabara kuu ya Tanzania-Malawi wakitokea wilayani Kyela kuelekea Mbeya.

"Walikuwa wanasafirisha bello 50 za vyandarua ambayo kila moja lina vyandarua 50 na hivyo jumla ya vyandarua walivyokuwa wanasafirisha kutoka Malawi, walikuwa wanasafirisha kwa kutumia gari mbili aina ya ya Toyota Noah zenye namba za usajili T.471 DDY na T.301 CTX," alisema Matei.

Hata hivyo Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi wa mali hizo kwa madai kuwa wana wasiwasi kuwa mzigo huo ulipatikana kwa njia za wizi. Alisema walifuatilia taarifa za mzigo huo na kubaini kuwa vyandarua hivyo vimetengenezwa mkoani Arusha na vilinunuliwa na Shirika la World Vission kwa ajili ya kupelekwa nchini Malawi lakini wahalifu hao wamevirejesha Tanzania.

Akizungumzia tukio hilo Meneja wa Forodha mikoa ya Mbeya na Songwe, Ginimasa Sindo, alisema endapo mzigo huo usingekamatwa Serikali ingepoteza zidi ya Sh. milioni 20 na hivyo akalishukuru Jeshi la Polisi kwa kuwakamata.

Alisema kwa sasa vyombo vyote vinavyohusika katika maeneo ya mipaka vinashirikiana kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayekwepa kulipa mapato ya serikali. Sindo aliwataka wafanyabiashara wote kuhakikisha wanapita katika vituo vya forodha ili walipie mali wanazosafirisha kutoka nje ya nchi ili wapate vibali na wasipate bughudha ya aina yoyote barabarani.

"Sisi hatupendi kuona mtu aliyetafuta pesa kwa jasho lake zinakuja zinakamatwa kama hivi, tunataka kila mtu apite kwenye vituo vyetu apate vibali ili kuepusha usumbufu barabarani," alisema Sindo. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alipongeza Jeshi la Polisi wilayani humo kwa kuendelea kudhibiti biashara za magendo katika wilaya yake kwa madai kuwa mbali na mali hizo pia kuna mali zingine zilizokamatwa hivi karibuni.

Alisema hivi karibuni Jeshi hilo pia lilikamata zaidi ya vifaranga 14,000 vikisafirishwa kutoka nchini Malawi kuingia Tanzania bila kibali, vitenge na mafuta ya kupikia.

Aliwataka wananchi kufuata taratibu za nchi wanapotaka kufanya biashara ya aina yoyote ikiwemo kupitia kwenye mamlaka za serikali kama TRA, TFDA NA TBS. Alisema kuwa kutokana na taarifa za vyandarua hivyo kutoeleweka vizuri, Serikali ya Tanzania itawasiliana na wenzao wa Malawi ili kujua walikovitoa na kujua uhalali wake.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, akionyesha baadhi ya bidhaa zilizokamatwa na jeshi hilo, baada ya kuingizwa nchini kwa njia za panya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# NMB yamwaga vifaa vya shule Ileje, Momba

**Na Mwamdishi Wetu,** SONGWE

WILAYA za Ileje na Momba mkoani Songwe, zimeziangukia taasisi na kampuni mbalimbali kujitokeza kusaidia miundombinu ya elimu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kuwahudumia wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Jumaa Irando, aliyasema hayo kwa nyakati tofati wakati akipokea msaada wa vifaa vya shule kutoka benki ya NMB ambayo ilitoa bati 254 kwa Halmahauri ya Tunduma Wilaya ya Momba na madawati 50 kwa shule za msingi Nyerere na viti 184 vya maabara kwa shule za sekondari za Ileje na Kafule zote za Wilayani Ileje huku vyote vikigharimu Sh. milioni 25

Irando alitoa rai hiyo jana huku akisema Mji wa Tunduma ni miongoni mwa miji inayokuwa kwa kasi kutokana na ongezeko la watu hivyo wamekuwa na changamoto lukuki kwenye suala la miondombinu ya shule.

Aliipongeza NMB kwa kuwaunga mkono ili kuhakikisha miundombinu ya shule inaboreshwa kupitia wadau mbalimbali.

"Kwa kweli tunachangamoto kubwa sana hapa Tunduma, kuna ongezeko kubwa la watoto wanaoanza darasa la kwanza kila mwaka tofauti na makisio au matarajio tunayokuwa tumejiwekea.

Jambo hili linasababisha msongamano katika shule mbalimbali kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati.

Alisema NMB imewaangalia kwa jicho la pekee na kutambua mahitaji yao huku akiwaomba wadau wengine waige hili jambo kwa ajili ya kuisadia jamii.

Alisema mahitaji ya huduma za kijamii ikiwamo afya na elimu yanahitaji kuungwa mkono na taasisi na mashirika mbalimbali ya kijamii kama inavyofanywa na benki ya NMB.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Joseph Mkude alisema imetekeleza wajibu wao na thamani yao kwa Watanzania hususani wananchi wa Ileje ambao kimsingi wapo pembezoni kabisa mwa nchi.

Alisema 'Nawashukuru sana NMB kutukubalia ombi letu na leo hii kutuletea sturi na madawati, kwetu sisi tunauthamini mno mchango wenu na katika hili tunazidi kuwaunga mkono kwa jitihada zenu, na tuwaahidi tutahakikisha vifaa hivi vinatunzwa ili vidumu kwa muda mrefu'.

Awali meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola alisema watambua umuhimu wa elimu na afya kwa Watanzania hivyo katika kipindi cha mwaka huu wa 2019, NMB imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya jamii ikiwamo afya, elimu na majanga ya dharula kwa nchi nzima.

Alisema benki hiyo itaendelea kusaidia katika sekta hiyo ikiwa ni sehemu ya kuunga juhudi za serikali za kuwahudumia wananchi wake. Alisema NMB ni wadau muhimu kwa Serikali na Watanzania hivyo wanao wajibu wa kuunga mkono juhudi za maendeleo kwa sababu jamii wanayoisaidia ndiyo inayowawezesha kupata faida katika biashara yao.

"Tunatambua changamoto ya elimu na afya, sisi NMB tunazipa kipaumbele sana kwa sababu hizi sekta mbili ni muhimu mno katika ustawi wa jamii yetu," alisema Chilongola.

## Waitaka Wizara ya Elimu kusitisha maswali ya kuchagua

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wameishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kusitisha maswali ya kuchagua kwenye mitihani ya kitaifa kwa madai kuwa maswali hayo yanadumaza uelewa wa mwanafunzi.

Wakizungumza kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika juzi mjini Igawa, madiwani hao walisema kuwa maswali hayo yanadumaza akili za wanafunzi na hivyo yahafai kuwa kipimo sahihi cha kuwafanya wasonge mbele kielimu.

Diwani wa Kata Mawindi, Yusuph Mhando alisema kuwa maswali ya kuchagua kwenye mitihani ya kitaifa pia yanachangia kuwafanya wanafunzi wasijisomee wakiamini kuwa mitihani hiyo ni rahisi kufaulu kwa kuchagua majibu.


Aliomba serikali kusitisha maswali ya kuchagua kwenye mitihani ya kitaifa kwa vile maswali hayo yanatoa mwanya hata wanafunzi wasio na uwezo kitaaluma ikiwamo kutojua kusoma na kuandika kufaulu mitihani hiyo.

"Naiomba Wizara ya Elimu isitishe maswali ya kuchagua kwenye mitihani wanayoandaliwa wanafunzi badala yake itunge maswali ya kujieleza ambayo ndiyo yanaweza kuwa kipimo kizuri kwa watoto wetu, haya maswali ya kuchagua ndiyo yanayosababisha hata mtoto hajui kusoma wala kuandika lakini ana kufaulu vizuri, alisema Diwani Mhando.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Oliver Sulle alipongeza juhudi kubwa zinazofanywa na madiwani katika kusimamia shughuli za maendeleo kwenye halmashauri hiyo na kuwataka waongeze bidii kwa ajili ya kuwaletea maendeleo zaidi wananchi wanaowaongoza.

Sulle pia alimpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kutatua migogoro ya Ardhi inayohusu mipaka na migogoro baina ya wananchi wanaoishi katika baadhi ya vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo imedumu kwa muda mrefu ndani ya Wilaya ya Mbarali.

Aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kusubiri maelekezo ya Serikali kabla ya kuanza kurudi kwenye maeneo hayo na kwamba wilaya hiyo ipo tayari kushirikiana na wananchi kuhakikisha maelekezo ya Rais yanafanyiwa kazi.





# Serikali yatangaza kupungua mauaji ya tembo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema kiwango cha mauaji ya tembo katika hifadhi za taifa kimepungua hadi kufikia 23 kwa mwaka 2018, tofauti na ilivyokuwa awali kati ya mwaka 2016 hadi 2017, ambapo waliuawa 194.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolph Mkenda, wakati akifungua mkutano wa kuwajengea uwezo vyombo vya ulinzi katika kukabiliana na ujangili kwa udhamini wa Palms Foundation.

Alisema katika kipindi hicho meno 211 na vipande 413 vya meno ya tembo vilikamatwa, silaha 355 na risasi zaidi ya 20,000 na hayo yote yalitokea kutokana na ushirikiano.

Profesa Mkenda alisema kulingana na kauli za wadau wa utalii katika mbuga ya Selou idadi ya wanyama katika hifadhi imeongezeka.

"Selou idadi ya wanyama imeongezeka, kwenye mbuga ya Ruaha wawekezaji wanakiri kuongezeka kwa idadi ya wanyama na kutaka jitihada zaidi kuongezeka ili kukabiliana na vitendo vya ujangili," alisema.

Aliwataka kuhakikisha wanapambana na ujangili na uharibifu katika sekta ya misitu na wanyama.

Alisema jitihada za kikosi kazi haziwezi kuzaa matunda bila kuungwa mkono na vyombo vya ulinzi na usalama. "Shime msilegeze kamba kutokana na mafanikio mliyofikia kwa kuwa wahalifu hawajachoka, wanabadili kila mbinu, mwendelee na uzi ule ule," alisema.

"Vijana wanawakamata wahalifu wanafunguliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani, wanapofika mahakamani wanakutana na changamoto, wahalifu wanaachiwa huru, lazima mkusanye vielelezo vya kutosha vya kesi na ushahidi wa kutosha ili kuwatia hatiani wahalifu na wapate hukumu stahili," alisema.

Mkurungezi wa Pams Foundation, Elisifa Ngowi, alisema wamekuwa wakipambana na vita dhidi ya ujangili kwa mafanikio na kwamba hatua hiyo ya kuungwa mkono na vyombo vyote vya dola.



Wadau wa sheria wakiwa kwenye uzinduzi wa jarida la taarifa za msaada wa kisheria wa wasaidizi wa kisheria lililotolewa Mjini Babati na mtandao wa asasi za kiraia mkoani Manyara (Macsnet), juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Fountain Gate yajitolea kusomesha mtoto aliyekatwa miguu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde, amemkabidhi katika Shule ya Fountain Gate Academy mtoto Christopher Alex (10), aliyekatwa miguu hivi karibuni baada ya kuugua ugonjwa wa ajabu ili atimize ndoto zake kielimu.

Juni 11, mwaka jana, Christopher alipatwa na maradhi hayo baada ya kufanyiwa tohara akiwa likizo akisoma darasa la pili katika Shule ya Msingi Mtitaa iliyoko wilayani Bahi.

Kutokana na hali hiyo, madaktari wa Hospitali ya Benjamin Mkapa walishauri mtoto huyo akatwe miguu baada ya kubaini hataweza kutembea kutokana na kuharibika.

Akimkabidhi shuleni hapo jana, Mavunde ambaye pia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, alisema ameamua kumsaidia mtoto huyo, ili aweze kutimiza ndoto zake kutokana na wazazi wake kutokuwa na uwezo wa kumhudumia kwenye hali ya ulemavu.

"Baada ya kufanyiwa upasuaji, wazazi wa Christopher walionekana kukata tamaa na wakaona ni mwisho wa maisha ya mtoto huyo, upande wa shule na kijamii kushirikiana na wenzake," alisema.

Alisema mtoto huyo amepatiwa miguu bandia na amemfanya kama sehemu ya familia yake kwa kumsomesha kwenye shule hiyo.

"Ile ndoto yake ya kupata elimu imetimia, tumemtoa Wilaya ya Bahi na wazazi wamekubali aje asome katika shule hii kubwa hapa Dodoma ya Fountain Gate, ambayo Mkurugenzi wake alionyesha utayari wa kumpokea katika shule ambayo kwa kweli inafanya vizuri na miundombinu yake ni rafiki kwa Christopher,"alisema.

Mavunde alisema mkurugenzi wa shule hiyo, ameamua kutoa mchango wake kwa kukubali mtoto huyo asome kwenye shule yake.

"Nitoe rai kwa Watanzania wawasaidie watoto wenye mahitaji kama Christopher, kwa kuwa ni sehemu ya shukrani kwa Mungu, nashukuru sana uongozi wa shule kwa kumpokea na kuanza masomo, tumelazimika kumrudisha darasa moja nyuma ili awe na uwezo kama wenzake," alisema.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Japhet Makau, alisema wameamua kumpokea kutokana na kumpa nafasi mbunge huyo kuleta watoto atakaoona wana mahitaji maalum kama Christopher ili watimize ndoto zao.

"Shule hii kwa sasa makao makuu yake yako Dar es Salaam, lakini tumeamua kuja Dodoma kwa sababu ni makao makuu ya nchi na kuna mahitaji mengi, hii ni miongoni mwa shule tano bora kwa Dar es Salaam, kusomesha watoto wenye mahitaji maalum ni azima yetu na kwa sasa tuna watoto yatima 20 na kila mwaka tunapokea wenye mahitaji maalum," alisema.

Naye mtoto Christopher alimshukuru Mavunde kwa kutimiza ndoto yake na kuahidi kusoma kwa bidii, ili baadaye aweze kuwa mwalimu.

# Wananchi wenye ujuzi waitwa kujenga mji wa serikali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANANCHI wenye ujuzi wa ufundi mbalimbali, wametakiwa kujitokeza kuchangamikia fursa za ajira katika mradi wa ujenzi wa mji wa serikali jijini Dodoma.

Wito huo, ulitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Idara ya Ujenzi, Ofisi ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Humprey Killo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa.

Killo aliwashauri wananchi wenye ujuzi wa ufundi pamoja na wasio na ujuzi huo, kujitokeza kuchangamkia fursa za ajira kwenye eneo hilo la mradi wa ujenzi.

"Mradi huu ni mkubwa, hivyo kila hatua inahitaji mafundi wenye ujuzi mbalimbali na kuwataka kujitokeza kuchangamkia fursa hii," alisema Killo.

Alitaja aina ya mafundi wanaohitajika kwenye mradi huo kuwa ni wenye fani ya umeme, uashi, ujenzi wa marumaru na wenye uwezo wa kupaua mapaa ya nyumba.

Alisema pia mafundi rangi, kuchomelea pamoja na wenye ufundi wa aina nyingine.

Aidha, aliwataka wananchi wengine hata wasio na ujuzi wa ufundi wanaweza kupata kazi za vibarua za kuwasaidia mafundi hao na kuweza kulipwa kwa siku.

Aliwataka wauzaji wa vifaa mbalimbali vya ujenzi kuchangamkia fursa hiyo.

Naye mamalishe Maimuna Kilemile, alisema kupitia mradi huo ameweza kunufaika kwa kuweza kuwauzia chakula mafundi na vibarua wanaofanya kazi za ujenzi katika eneo hilo.

Kilemile alisema katika eneo hilo kuna maeneo mengi yanayojengwa, hivyo kila kundi linaweza kufika maeneo hayo kutoa huduma na kujipatia ajira na kipato.

Kaimu Meneja TBA Kanda ya Kati, Herman Tanguye, alisema wakala huo ulipewa kazi ya kutekeleza ujenzi wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao umefikia hatua ya kupaua jengo.

Tanguye alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakamilisha mradi wa ujenzi huo ifikapo Februari 14, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Serikali yamwagiwa pongezi kwa kusamehe deni la ZECO

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi Zanzibar, kimepongeza hatua ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuta deni la Sh. bilioni 22 ambalo Serikali ya Zanzibar ilikuwa inadaiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Catherine Peter Nao, alisema kuwa hatua hiyo ni ya kupongezwa kwa kuwa deni hilo lilikuwa kubwa na lilikuwa ni changamoto kwa Zanzibar.

"Deni hilo lilikuwa ni mzigo mkubwa kwa Zanzibar, hivyo tunawapongeza kwa dhati viongozi wetu," alisema.

Alisema hatua hiyo iliyofanywa na Baraza la Mawaziri chini ya mwenyekiti wake, Rais John Pombe Magufuli, ni matunda ya muungano uliopo sasa.

"Imani yetu kwamba CCM 2020 itavuka salama katika uchaguzi wa mkuu kutokana na mambo mazuri yanayofanywa na Rais wetu,"alisema.

Ofisa Uhusiano wa ZECO, Salum Abdallah, alisema kuwa deni lililofutwa ni kodi, ambapo Zanzibar haikuwahi kulipa tangu kusainiwa kwa sheria ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Alieleza kuwa kufutwa kwa deni hilo haina maana ya kwamba bei ya umeme sasa itashindwa.

Aidha, alisema kuwa licha ya kwamba deni hilo limefutwa, lakini bado ZECO inadaiwa na Tanesco deni la matumizi ya umeme wastani wa Sh. bilioni 18.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akiangalia zao la uyoga kutoka kwenye kikundi cha ujasiriamali, Kata ya Ndembezi, mjini Shinyanga, kikundi hicho ni kati ya kilichoshindwa kurejesha marejesho ya mikopo katika manispaa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri amwaga ushauri kwa bodi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashidi Mohamed, ameishauri Bodi ya Ushauri ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kuangalia uwezekano wa kuvitumia vifaa tiba vilivyoko kwa ajili ya kazi nyingine za utafiti wa kisayansi.

Alisema wizara inavyo vifaa vingi vya tiba ambavyo havijatumika kikamilifu na vinaweza kusaidia kwa shughuli nyingine mbalimbali za maendeleo zikiwamo za utafiti.

Waziri Hamad alieleza hayo katika hafla ya uzinduzi wa Bodi ya Pili ya Ushauri ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, iliyofanyika jengo jipya la ofisi hiyo eneo la Maruhubi Mjini Zanzibar.

Alisema kitu muhimu kwa bodi hiyo ni kuongeza ubunifu na kuzaa mawazo mapya ambayo yataweza kusaidia kuongeza matumizi kwa baadhi ya vifaa ambavyo vimekuwa vikitumika kwa muda mchache na uwezo wa kutumika ni mkubwa.

Waziri huyo aliitaka bodi hiyo kutoa kipaumbele suala la rasilimali watu kwa kuwatafutia masomo wafanyakazi wanaosimamia mashine za maabara hiyo kwa kuwa teknolojia inabadilika.

Aliitaka bodi kujiandaa kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule, ili waelewe umuhimu wa sayansi katika maendeleo ya taifa.

Katika kujenga utashi wa kisiasa, Waziri Mohammed ameishauri bodi hiyo kutoa elimu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na makundi mengine ya kisiasa, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa bodi kusimamia matumizi bora ya mashine ya maabara hiyo, ili ziweze kudumu muda mrefu ujao.

Alisema serikali imetumia fedha nyingi kununua mashine za maabara hiyo, ikiwamo ya kuchunguza vinasaba vya watoto wanaozaliwa ambayo kwa miaka mingi ilikosekana Zanzibar.

Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo, Dk. Haji Mwemvura Haji, alimhakikishia Waziri Mohammed kwamba maelekezo yote yaliyotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, alipolifungua jengo hilo hivi karibuni yatatekelezwa.

Dk. Mwemvura alimshukuru Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi hiyo, Dk. Yussuf Nuhu, kwa kazi kubwa aliyoifanya na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## Serikali yakerwa mpangilio mbovu wa vibanda

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema hairidhishwi na mpangilio mbaya wa vibanda vya biashara katika masoko ya Mombasa na Mwanakwerekwe.

Akizungumza katika ziara aliyofanya kwenye masoko hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, alisema hali hiyo inachangia kuongezeka kwa uchafu katika masoko hayo.

Alieleza kuwa, uchafu uliokithiri katika masoko hayo, umekuwa kero kwa wafanyabiashara na wageni wanaofika humo kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa mbalimbali.

Alisema wafadhili walijenga masoko hayo kwa mpangilio maalum wa njia na maeneo ya wazi, hivyo si vyema kubadilisha utaratibu huo na kuharibu mwonekano wake wa asili.

Aidha, alisema mpangilio mbaya husababisha mrundikano wa wafanyabiashara na hivyo kupoteza mapato.

Waziri Kheri alieleza kushangazwa kwake kwa sehemu zilizokuwa za wazi katika masoko hayo kushamiri vibanda na kuleta usumbufu kwa magari yanayoingiza bidhaa katika masoko hayo.

"Nashangaa kuona sehemu zote zilizokuwa za wazi katika masoko, sasa yanaonekana kushamiri vibanda na kuleta usumbufu kwa watumiaji wa soko," alisema.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa mitaro ya maji taka, Waziri Kheir, aliyaagiza Mabaraza ya Manispaa kuhakikisha inachukua juhudi za ziada kuisimamia na kuisafisha ili iwe endelevu kwa kuwa serikali imetumia gharama kujenga miundombinu hiyo.

Katika hatua nyengine waziri huyo alipongeza uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa jitihada kubwa za kuendeleza bustani katika maeneo mbalimbali ya manispaa ya mji huo na kuzitaka manispaa nyingine kuendelea na utaratibu huo katika maeneo yao.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema hatawavumilia wale wote wanaoharibu mazingira ya mji na kusababisha uchafu, hivyo sheria kali zitachukuliwa dhidi ya watu watakaobainika kutenda mambo hayo.

# Mwanafunzi huru adhabu ya kifo

**KHARTOUM,** Sudan

MAHAKAMA ya Sudan imemfutia mashtaka na kuamuru kuachiliwa huru mwanafunzi mmoja wa Chuo Kikuu cha Khartoum, aliyeshtumiwa kumuua polisi wakati wa maandamano ya mwaka 2016.

Wakati wa kesi yake ya mwanzo alihukumiwa kifo, kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Haki za Binadamu la Amnesty.

Asim Omer, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Khartoum, alikamatwa Desemba 2016 na kushtakiwa kwa mauaji ya polisi wakati wa makabiliano kati ya mamia ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Khartoum na vikosi vya usalama mwezi Aprili, 2016.

Asim Omer ambaye ni mfuasi wa chama cha Popular Congress Party (PCP), ambacho kinashiriki serikalini, alihukumiwa kifo Septemba 2017. Uamuzi huo wa mahakama ulizua maandamano makubwa ya wanafunzi wa chuo kikuu hicho mbele ya mahakama. Maandamano ambayo yalisambaratishwa na vikosi vya usalama kwa kutumia gesi ya machozi.

Awali, Mahakama ya Rufani iliamuru kesi hiyo irejelewa upya na Jumanne wiki hii, mahakama ilimfutia mashtaka Asim Omer na kuamuru aachiliwe huru, kwa mujibu wa Amnesty International na taarifa ya chama cha PCP.

Amnesty International limekaribisha uamuzi huo, huku ikitolea wito mamlaka kuchunguza madai kwamba Asim Omer "aliteswa gerezani." **RFI**

# Kima cha chini juu Nigeria asilimia 50

**ABUJA,** Nigeria

SERIKALI ya Nigeria imeongeza asilimia 50 ya mshahara wa chini, baada ya miezi kadhaa ya mvutano na vyama vya wafanyakazi na vitisho vya mgomo, Waziri wa Kazi, Chris Ngige, amesema.

Mshahara wa chini, Nigeria yenye idadi kubwa zaidi ya watu barani Afrika ni naira 18,000 (sawa na chini ya euro 44) kwa mwezi kwa wafanyakazi katika sekta ya umma na ya kibinafsi.

Novemba mwaka jana, wakuu wa majimbo walifutilia mbali mkataba wa kiwango cha naira 30,000, wakisema "haiwezekani", huku wakipendekeza kupunguzwa kwa watumishi wa umma au kuongeza bajeti wanayotengewa kutoka serikali ya shirikisho.

Licha ya marupurupu ya kila mwezi kutoka serikali ya shirikisho, majimbo mengi hayajalipa wafanyakazi wao kwa muda wa miezi kadhaa, na kusababisha mdororo wa uchumi kwa taifa hilo kubwa Afrika Magharibi tangu 2016.

Waziri wa Kazi aliwaambia waandishi wa habari kwamba jumla ya kiwango cha "(naira) 27,000 kimeidhinishwa", kufuatia mkutano wa Baraza la Kitaifa la Majimbo. **RFI**

# Italia yawataka Wafaransa wamwondoe Rais Macron

**ROMA,** Italia

MZOZO wa kidiplomasia na kisiasa unazidi kufukuta kati ya wanachama wawili waanzilishi wa Umoja wa Ulaya, Italia na Ufaransa na sasa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Italia anatoa wito kwa Wafaransa kumwondoa Rais Emmanuel Macron.

Juzi Waziri wa Mambo ya Ndani wa Italia, Matteo Salvini, alitumia ukurasa wake wa Facebook kumshambulia vikali Rais Macron, akimwita rais mbaya sana anayependa maneno, lakini asiye na matendo. Salvini anayeongoza chama kinachopinga wahamiaji, amemtuhumu Macron kwa kuipa darasa Italia na kumtaka badala yake awaruhusu wahamiaji walioko kwenye mpaka wa nchi yake na Ufaransa.

"Ikiwa kweli Macron ni mzuri, hivyo anaweza kuthibitisha kwa kuwaruhusu maelfu ya wakimbizi waliopo Italia na ambao aliwaahidi ukarimu pamoja na mataifa mengine ya Ulaya. Si suala la Matteo Salvini kuingia siasa za Ufaransa, lakini natarajia wananchi wa Ufaransa hapo tarehe 26 Mei, watamchagua mtu mwingine anayewawakilisha zaidi, aliye makini zaidi, aliye wa matendo zaidi. Namfikiria mtu kama Marine Le Pen," alisema Salvini.

**Vuguvugu la Nyota Tano la Di Maio linaunga mkono vuguvugu la Vizibao Manjano nchini Ufaransa linaloipinga serikali ya Rais Macron.**

Lakini akimjibu Salvini, waziri anayeshughulikia masuala ya Ulaya katika serikali ya Ufaransa, Nathalie Loiseau, alisema Wafaransa walikuwa na muda wa kuchaguwa baina ya Le Pen na Macron na wakafanya chaguo lao. Akitumia mtandao wako wa Twitter, Loiseau aliandika: "Matteo Salvini anawatukana Wafaransa. Wataliano wanafaidika nini? Hawafaidiki kitu. Je, matusi haya yanabadili kitu kwenye siasa za Ufaransa? Hapana!"

Wakati serikali ya Italia ikikabiliwa na lawama kwa vifo vya wahamiaji kadhaa vilivyotokea hivi karibuni kwenye Bahari ya Mediterania, Naibu Waziri Mkuu, Luigi Di Maio, alijaribu Jumapili iliyopita kuzihamishia lawama hizo kwa Ufaransa.

Di Maio alisema Ufaransa ilitumia sera za kikoloni barani Afrika, ambazo ziliwatia ufukara Waafrika na kuwafanya sasa wakimbilie pwani za Ulaya.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ilimwita balozi wa Italia siku ya Jumatatu kutokana na kauli hiyo.

Vuguvugu la Nyota Tano la Di Maio linaunga mkono vuguvugu la Vizibao Manjano nchini Ufaransa linaloipinga serikali ya Rais Macron.

Juzi Waziri Mkuu wa Italia, Giuseppe Conte, alisema kuwa mzozo wa wakimbizi hautishii urafiki wa kihistoria kati ya mataifa hayo mawili majirani, akisema kuwa mahusiano yao yataendelea kusalia madhubuti na imara, licha ya mzozo huu wa kisiasa. **DW**



Askari wa vikosi vya usalama vinavyolinda mpaka wa India (BSF) wakiendesha pikipiki kushiriki mazoezi ya gwaride la kuadhimisha siku ya Uhuru jijini New Delhi, jana. **PICHA: REUTERS**

# Tshisekedi kuapishwa kuiongoza Congo?

**KINSHASA,** DRC

KUNA uwezekano kuwa Rais Mteule wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, huenda akaapishwa leo kwenye makao makuu ya Bunge, vyanzo vilio karibu na ofisi ya rais vimebainisha.

"Sherehe za kutawazwa kwa rais mpya zitafanyika Alhamisi (leo) saa sita mchana," mshauri mkuu wa Joseph Kabila anayehusika na masuala ya kidiplomasia, Barnaba Kikaya Bin Karubi, alisema kwa mujibu wa Kitengo cha Afrika cha Sauti ya Marekani (VAO Afrique).

Mshauri mwingine wa Rais Kabila pia amethibitisha taarifa hizo, akisema sherehe itafanyika kwenye makao makuu ya Bunge la taifa, "sherehe ambayo itahudhuriwa na marais kadhaa wa nchi za Afrika."

Ni kwa mara ya kwanza nchi hiyo itashuhudia kuapishwa kwa rais mpya aliyechukua madaraka kwa njia ya amani kutoka kwa rais mwingine.

"Ulimwengu utashuhudia sherehe kubwa ya kukabidhiana madaraka kwa amani, kinyume na jinsi wengi walivyofikira," alisema mshauri mwingine wa Kabila. Lakini hakuna taarifa rasmi iliyowekwa wazi kuhusu maelezo ya sherehe hiyo.

Timu ya rais mpya na ile ya rais anayemaliza muda wake wamekuwa wakijadili eneo na tarehe ya sherehe hiyo muhimu nchini DRC, vyanzo hivyo vimeongeza.

Mbali na marais hao wa nchi za Afrika, Ufaransa na Marekani zitawakilishwa katika sherehe hiyo na mabalozi wao. Jumanne Rais mpya aliyechaguliwa Felix Tshisekedi alikutana na balozi wa Marekani. **RFI**

# Mvua ya dakika 30 yatikisa msafara wa RC

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MVUA iliyonyesha kwa dakika 30 jana, ilisababisha msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nickodemas Mwangela, akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kukwama kwa saa mbili.

Msafara huo ulikwama kutokana na maji kupita kwa kasi juu ya daraja la mto Mkota, huku madereva wakihofu magari kusombwa na maji.

Msafara huo ulikuwa ukitokea makao makuu ya mkoa kuelekea Wilaya ya Songwe kukagua miradi ya maendeleo ikiwamo Kituo cha Afya cha Magamba Kata ya Magamba, kitakachohudumia wakazi zaidi ya 75,000 kutoka katika kata sita, ambazo awali walikuwa wanasafiri kilometa 20 kusaka huduma za matibabu.

Hata hivyo, baada ya saa moja na nusu maji yalipungua ndipo msafara uliendelea na ukaguzi kufanyika.

Kapala Makelele, Diwani wa Kata ya Magamba, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia wakazi wa kata za Kanga, Namkukwe, Ifwenkenya, Totoe na Galula, ambao idadi yao inazidi 75,000, walikuwa wakitembea zaidi ya kilometa zaidi 20 kufuata tiba katika Hospitali Teule ya Mwambani.

Alisema amewahi kushuhudia vifo vingi vya wazee, watoto na wajawazito waliokuwa wakivuka mito kwenda hospitalini kupata matibabu ,wakivuka mito mikubwa mitatu na kwamba serikali imesikia kilio cha wananchi na imepeleka Shilingi milioni 400 kujenga kituo cha afya kunusuru wananchi.

Victor Madamila, ofisa takwimu wilayani humo, kwa niaba ya mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo, alisema mwaka wa fedha 2017/18, halmashauri ilipokea Shilingi 400,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Hata hivyo, Madamila alisema fedha iliyotumika ni Shilingi 120,633,000, na kwamba wananchi walichangia Shilingi 279,367,000.

Aliwapongeza wakazi wa Magamba kwa kujitoa kwa hali na mali na kuchangia nguvu kazi hasa katika kuchimba msingi, kusomba mawe na mchanga kwa nguvu zao zilizoongeza thamani kufikia Shilingi 5,900,000. Hadi sasa fedha taslimu zilizochangwa ni Shilingi 15,476,000.

Mhandisi wa ujenzi wa ujenzi wa halmashauri hiyo, Mhandisi Cyrille Mkombozi, alisema ujenzi unaendelea vizuri na mradi upo asilimia 70 na kwamba ulianza tarehe Machi 1, mwaka jana na unatarajia kukamilika Machi mwaka huu, huku akisema changamoto ya mvua imesababisha usafiri wa kusafirisha vifaa vya ujenzi kuwa mgumu.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samwel Jelemiah, alisema wamejifunza mengi kuhusu usimamizi wa miradi na kudai kuwa ujenzi utakamilika kama ulivyo pangwa licha ya usafirishaji wa vifaa kuwa mgumu kutokana na mvua za masika zinavyoendelea kunyesha.

Naye Mkuu wa Mkoa, Brigedia Jenerali Mwangela, alipongeza ujenzi unavyoendelea kwa kasi na ubora kisha kushauri vifaa vya ujenzi vinunuliwe na kusafirisha kwa pamoja ili zisiwapo sababu za kuchelewesha kwa mradi kwa kisingizio cha mvua.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga na Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg, wakibadilishana nyaraka baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano baina ya ubalozi huo na kituo hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mashahidi wakwamisha kesi daktari feki

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma, imeahirisha kesi ya mtu anayedaiwa kujifanya daktari, Maximillian Martin (40), mkazi wa Makere aliyekuwa akifanya kazi Red Cross katika kambi ya wakimbizi Nyarugusu, Wilaya ya Kasulu baada ya upande wa mashtaka kudai kuwa mashahidi wake wako safarini.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mutembei, akikabiliwa na makosa matano ya kughushi cheti cha shahada, cheti cha mafunzo kwa vitendo, cheti cha usajili kutoka Baraza la Madaktari wa Tanganyika, kufanya shughuli za udaktari wa binadamu kinyume cha Sheria ya madaktari sura namba 152 ya mwaka 2002 na kufanya shughuli za udaktari wa binadamu kinyume cha sheria ya madaktari namba 11 ya mwaka 2017.

Awali mshtakiwa huyo aliposomewa mashtaka yake alikana yote na yuko nje kwa dhamana ya watu watatu na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni nane.

Awali upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Benedict Kivuma, ulisema kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kueleza kuwa upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mashahidi 13 pamoja na vielelezo 10.

Mshtakiwa huyo anatetewa na wakili wa kujitegemea, Medhod Kabuguzi.

Kivuma alidai kuwa katika kesi hiyo mashahidi watatu wameshatoa ushahidi wao na vielelezo vinne na kubaki mashahidi 10 na vielelezo sita.

Hakimu Mutembei aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 5, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine.

# Wanne kortini tuhuma za wizi wa ng'ombe

**Na Enock Charles**

WAKAZI wanne wa Chanika Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, wameshtakiwa katika mahakama ya Ilala kwa kosa la kuiba ng`ombe eneo la Kigezi Chanika, mali ya Lucy Christopher.

Watuhumiwa hao Agustino Mathias ,Prosper Constantine, Shukuru Thomas na Manyori Malala inadaiwa Aprili 13, mwaka jana katika eneo la Kigezi Chanika waliiba ng`ombe mwenye thamani ya Sh. 800,000.

Akitoa ushahidi mbele ya Hakimu Catherine Kioja, Afisa Upelelezi wa Jeshi la Polisi wa kituo cha polisi Chanika, Warioba, alidai ngombe huyo alipangwa kuuzwa Aprili 12, mwaka jana, lakini siku iliyofuatwa alikutwa ameibwa na kuchinjwa, na kuwa watuhumiwa hao walikamatwa baada ya polisi kuweka mtego.

Afisa huyo alitoa vielelezo ambavyo ni vifaa mbalimbali vilivyotumika katika wizi huo ambavyo ni begi moja lililokuwa na kisu, nondo, kopo moja la spray lililoelezwa kuwa na sumu, raba na tisheti na kuomba vipokelewe mahakamani kama uthibitisho.

Alipoilizwa na hakimu kuhusu vitu hivyo, mshtakiwa wa pili, Prosper Constantine alikana kulitambua begi hilo.

Mwendesha Mashtaka wa mahakama hiyo Grace Mwanga, aliomba mahakama ivipokee vielelezo hivyo na hakimu alikubali, hivyo kupokelewa.

# Japan yamaliza changamoto madarasa

**Na Futuna Seleman**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Sophia Mjema, amesema kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa madarasa katika Shule ya Msingi Gogo, Kata ya Zingiziwa, utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi wa darasa la kwanza katika shule hiyo.

Aidha, alisema ujenzi huo utapunguza utoro kwa wanafunzi, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza pia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Aliyasema hayo baada ya kukabidhiwa jengo la ofisi ya walimu lenye thamani ya Dola za Marekani 94.5 kutoka Serikali ya Watu wa Japan pamoja na madarasa matatu kwa ajili ya Shule ya Msingi Gogo iliyopo Kata ya Zingiziwa, wilayani Ilala. Balozi wa Japan nchini Tanzania, Shiniti Goto, alimkabidhi msaada huo Mkuu wa Wilaya kwa niaba ya Serikali Kuu. Mjema alisema msaada huo utaimarisha uhusiano mwema kati ya Serikali ya Tanzania na Japan.

Mkurungezi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri, alisema mradi wa upanuzi wa shule hiyo ulianza Mei 2018 kwa ufadhili wa Serikali Japan, halmashauri pamoja na jamii.

Balozi wa Japan nchini Goto, alisema mradi huo utasaidia kutoa mazingira mazuri ya kusoma pamoja na kufundishia na Shule hiyo itakuwa mfano kwa Shule zingine.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## NYUMBA/VIWANJA


**NYUMBA SELF CONTAINER INA FENCE MAJI NA UMEME INAPANGISHWA** ipo Segerea kwa bibi bei 3.6 milion kwa N0754467237/0754284708


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## CHETI KIMEPOTEA



**PHINIAS OPANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0136-084** kilichotolewa na MUSOMA SEKONDARI mwaka 1991.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KJN/B.I/I/VOL/499/2019.**

115022302

## KUPOTEA KWA CHETI



**Carolina Shayo** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0332/0010** kilichotolewa na shule ya Sekondari Morogoro mwaka 1989. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **MS/RB/705/2019**

115021002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AFRICAN POWER MACHINERTTIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye namba za usajili T. 155 DFJ. Chassis namba AZR600225121.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **ILA/RB/99543/2019.**

115022402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AMINA RAMADHANI HASSAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya BMW yenye namba za usajili **T 777 DMX.** Chassis namba **WBAPA7206OWB69485.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/IR/RB/8230/2018.**

115021602

**IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.82 OF 2018**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE PAUL ALEX MALLYA - DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ELIZABETH PAUL MALLYA.**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of probate for letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 13 day of **February, 2019.**

The will if any of the said deceased to be deposited and open for inspection of the Court.

Dated 23rd This day of January 2019.

115021702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Sakina Express Co. Ltd** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T990 BUV**, Aina ya TRAILER yenye chasis namba **C104275**. Yeyote atakaeiona atume taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KOB/RB/281/2019**

115021102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FAUSTINE VALENTINE MOSHA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T967 CDK** MITSUBISHI Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **AR/RB/626/2019**

115021402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**TUMAINI UNIVERSITY STUDENTS ORGANISATION (TUSO-IUCO).** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T.191 AJH** Aina ya **TOYOTA COASTER** yenye chassis namba **JT 743PB5108000877** na Engine namba **1h20129050.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya Polisi. **IR/IR/RB/316/2019.**

215021502


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***0767 223311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***
***Tupigie 0767 223 311***


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# REAL WAJIANDAA KUMNG'OA DYBALA JUVENTUS




**TURIN,** Italia

REAL Madrid itatoa ofa ya paundi milioni 90 kwa ajili ya kumsajili Paulo Dybala kutoka Juventus kipindi kijacho cha majira ya joto, huku wakipanga kupiku matumaini ya Manchester City ya kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Argentina.

Los Blancos hao wamekuwa hawana safu imara ya kufunga mabao baada ya kumuuza nyota wao Cristiano Ronaldo kwenda Juventus mwaka jana, na wanaamini kwamba Dybala anaweza kuwa suluhisho la upatikanaji wa mabao.

Gazeti la The Sun limedai kwamba hilo litakuwa pigo kwa Pep Guardiola, ambaye amekuwa shabiki mkubwa wa Dybala kwa muda mrefu na amekuwa akimwania kumchukua kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji ya Manchester City.

Licha ya kubainisha kwamba City haiwezi kuingia kwenye vita ya kugombea wachezaji kwenye usajili, Guardiola hivi karibuni aliweka wazi kuwa Real Madrid ni klabu ambayo hawezi kushindana nao kwenye soka la usajili.

"Kama unakuwa peke yako unamtaka mchezaji ni rahisi," alisema. "Lakini kama ukimtaka mmoja au wengi, klabu nyingi zinamtaka zaidi, ni vigumu hasa kwa timu kama Madrid au Barcelona.

"Kwa kawaida ukiingia kwenye vita ya kuwania usajili wa wachezaji na Madrid na Barcelona ni lazima utashindwa. Unakuwa huna nafasi."

Baada ya kufunga mabao 22 kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, Dybala amefunga mabao mawili tu hadi sasa kwenye Ligi, akiwa amepitwa na Ronaldo, ingawa amefunga mabao matano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Juventus inaweza kumuuza Dybala mwishoni mwa msimu huu, huku ikitaka kuimarisha safu yake kwa kuwasili kwa Aaron Ramsey kutoka Arsenal.

Kiungo mshambuliaji wa Real Madrid, Isco, akiwa hana nafasi chini ya kocha, Santiago Solari pale Real Madrid, anaweza kujiunga na Juventus.

## *Barca wakaribia kumsajili de Jong*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KIUNGO wa kimataifa wa Uholanzi, Frenkie de Jong, amechagua kujiunga na Barcelona, huku maofisa wa miamba hao wa Catalunya wamepaa kwenda jijini Amsterdam Jumatano kukamilisha uhamisho huo.

Nyota huyo wa Ajax amekuwa mchezaji aliyetajwa zaidi kwenye dirisha hili dogo la usajili, huku pia akiwa amehusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Manchester City na Paris Saint-Germain.

Hata hivyo, redio Catalunya Jumanne ilisema kwamba de Jong ameamua kujiunga na Barcelona ambao ni miamba wa Ulaya mwezi huu.


Ujumbe wa klabu ya Barcelona ilisafiri kwenda Uholanzi Jumatano kwa ajili ya kukamilisha usajili huo wa kutua pale kwenye dimba la Camp Nou.

Imedaiwa kwamba, wakala wa de Jong tayari amefanya mazungumza na klabu nyingine ikiwamo Paris Saint-Germain, kuwajulisha kuwa mipango ya mchezaji huyo ameamua kuhamia Barcelona.

Ofisa Mtendaji wa Ajax, Edwin Van Der Sar, awalia alidai kwamba klabu isingeweza kumuuza mchezaji wakati huu wa kipindi hiki cha dirisha la dogo la Januari, lakini ada yake ya paundi milioni 79 imetajwa kuwa inamfanya kuwa mchezaji ghali zaidi wa Uholanzi kusajiliwa.

Gazeti la The Express limebainisha kuwa mshahara wa de Jong utakuwa ni paundi milioni 14 kwa mwaka akishajiunga na klabu hiyo.

De Jong amecheza mechi 16 kwa Ajax msimu huu, akifunga mabao manne na kuisaidia timu yake kuongoza msimamo wa pointi nne zaidi.



## Man Utd yakataa kumtoa Bailly kwa Arsenal

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United inaamini kwamba imekataa ofa kutoka Arsenal kwa ajili ya beki wa kati, Eric Bailly, kwa mkopo kwa kipindi kilichobaki cha msimu huu.

Kocha huyo raia wa Ivory Coast amecheza mara chache kwa mashetani wekundu hao msimu huu, na amecheza mara moja tu chini ya kocha wa muda, Ole Gunnar Solskjær, kwenye mchezo ambao alitolewa nje kwa kadi nyekundu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alisajiliwa na José Mourinho mwaka 2016 kwa ada ya uhamisho ya paundi milioni 30, na kwa sasa amebakiza miezi 18 kwenye mkataba wake.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, kocha wa Arsenal, Unai Emery, amejaribu kutaka kumleta mchezaji huyo wa zamani wa Villarreal hapo kwenye dimba la Emirates kwenye mkataba wa muda mfupi.

Hata hivyo, washika bunduki hao na United wameshindwa kufikia makubaliano kwa ajili ya kumsajili Bailly.

Huku Arsenal ikikabiliwa na majeruhi baada ya Rob Holding na Héctor Bellerín wakiwa majeruhi ya goti, Emery anapigania kuhakikisha kwamba anapata wachezaji wanaoweza kumpitisha kwenye kipindi hiki.





# HENRY: NAHOFIA MAJALIWA YA MONACO

**MONACO,** Ufaransa

KOCHA wa Monaco, Thierry Henry amesisitiza kwamba anafikiria zaidi kuhusu majaliwa ya timu yake kuliko yeye mwenyewe.

Ikiwa inajikongoja kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Monaco pia imetolewa kwenye kombe la Coupe de France kwa kuchapwa 3-1 na Metz Jumanne iliyopita.

Henry alichukua nafasi ya kuinoa klabu yake hiyo ya zamani Oktoba mwaka jana, lakini bado hajaweza kuirudisha kwenye reli klabu hiyo yenye matokeo mabaya msimu huu.

Hata hivyo, Mfaransa huyo amesema maamuzi yoyote juu yake kuhusu majaliwa yake yako mikononi mwa wamiliki wa klabu hiyo, kwani yeye akili yake anaifikiria zaidi Monaco.

"Majaliwa yangu? Wamiliki wanaweza kuamua wakati wakihitaji kuamua. Nahofia zaidi majaliwa ya Monaco. Nimeshasema hivyo," amesema Henry akiwaambia waandishi wa habari.

"Nitaheshimu maamuzi. Haihitaji mara zote kuuliza swali hilohilo, na nitajibu hivyo hivyo.

"Atletico Madrid waliwahi kushuka daraja miaka ya 90 wakiwa na kikosi imara kuliko sisi. Vilecile Real Zaragoza walishuka hivi karibuni. Naweza kuzungumza lugha zote.

# Guardiola: Otamendi hana furaha Man City

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekubali kwamba Nicolas Otamendi hana furaha hapo Manchester City kwa sababu ya kukosa nafasi ya kucheza.

Otamendi anapigania namba na nahodha wa Man City, Vincent Kompany, beki wa England, John Stones awali alikuwa anawania pamoja na beki wa kati aliyeweza rekodi ya usajili klabuni hapo, Aymeric Laporte.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, ameanza katika mechi nane tu za Ligi Kuu msimu huu, huku akikaa kwenye benchi kwenye mechi 13.

"Hana furaha - sina jibu lake," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati anapocheza anakuwa na furaha, wakati anaposhindwa kucheza hana furaha. Sijui nini ninachoweza kufanya. Wakati anaposhindwa kucheza anakuwa na furaha.

"Hawezi kucheza kila wiki, anaweza kucheza najua wapi alipo. Anaweza kutusaidia kuijenga timu. Nina mabeki wa kati wa tatu na pamoja na Kompany. Alicheza dhidi ya Southampton vizuri zaidi.

"John alikuja vizuri baada ya kombe la Dunia, anataka kucheza mechi zaidi. Najua kwamba Nico anaweza kucheza na analipenda hilo."

Mwisho.





# Sala alituma ujumbe kabla ndege kupotea

**GUERNSEY,** England

MSHAMBULIAJI mpya wa klabu ya Cardiff City aliyeweka rekodi ya usajili ndani ya timu hiyo, Emiliano Sala, alipata nafasi ya kutuma ujumbe mfupi wa sauti ndani ya ndege kwa baadhi ya ndugu na marafiki zake kupitia mtandao wa 'WhatsApp' kabla ya ndege yake kupotea.

Mshambuliaji huyo raia wa Argentina alisajiliwa Jumamosi akitokea klabu ya Nante ya Ufaransa kwa dau la paundi milioni 15 na kupanda ndege kuelekea Cardiff kabla ya kupotea kwenye rada mara baada ya kufika umbali wa maili 12 kutoka Kaskazini mwa Kisiwa cha Guernsey siku ya Jumatatu.

"Nipo ndani ya ndege muda huu naelekea Cardiff, kesho nitaanza mazoezi na timu yangu mpya. Lakini inaonekana kama ndege itaanguka," alisema Sala kupitia ujumbe wa sauti aliyoiutuma kwa marafiki zake kupitia mtandao wa WhatsApp kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Sala ameongeza, "Kama hutopata habari zangu zozote ndani ya saa moja na nusu sioni kama kuna sababu ya kumtuma mtu wa kunitafuta, nimejawa na hofu."

Mapema jana polisi wa visiwa vya Guernsey walitoa taarifa ya kuahirisha zoezi la kuendelea kumtafuta mchezaji Sala, huku kukiwa hakuna ishara yoyote ya kupatikana kwake baada ya ndege ndogo aliyokuwa akisafiria kupotea.

Mamlaka ya anga ya Ufaransa ilithibitisha Jumanne wiki hii kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alikuwa kwenye ndege ndogo ambayo ilipotea kwenye rada ambayo ilikuwa inatoka Nantes kwenda Cardiff Jumatatu.

Sala, ambaye alithibitisha kwamba ndiye mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi kwa Cardiff Jumamosi baada ya kuamua kuondoka Ligue 1 katika klabu ya Nantes, na inadaiwa ndege hiyo ya injini moja ilikuwa na watu wawili.

Timu ya uokozi ilifanya kazi hiyo usiku kucha, lakini polisi wa Guernsey wamethibitsha kwamba wasingeweza kuendelea na zoezi hilo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PIGO SPURS, DELE ALLI NAYE NJE HADI MACHI

## ●●● Alipatwa na majeraha hayo Jumapili wakati wa mechi dhidi ya Fulham...

**LONDON,** England

TOTTENHAM imepata pigo kubwa katika safu yake ya ushambuliaji kufuatia kuandamwa na majeruhi baada ya winga Dele Alli kukumbwa na majeraha ya misuli ambayo yatamweka nje ya uwanja hadi mapema Machi mwaka huu.

Alli alipatwa na majeraha hayo Jumapili wakati wa mechi dhidi ya Fulham na taarifa hizo za kuwa nje ya uwanja zimekuwa ni pigo kwa Spurs, ambayo tayari ilishampoteza mshambuliaji Harry Kane hadi Machi baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati wa mechi dhidi ya Manchester United.

Son Heung-min pia hayumo na kikosi hicho kutokana na kuwa na majukumu na timu yake ya Taifa ya Korea Kusini kwenye michuano ya Kombe la Asia.

**Kuumia kwa Alli, kutamfanya akosa mechi nyingi muhimu za kikosi hicho cha Mauricio Pochettino, ambacho kinakabiliwa na mechi ya nusu fainali ya marudiano ya Kombe la Ligi ('EFL Cup') dhidi ya Chelsea Alhamisi, wakati huu kikishikilia ushindi wa bao 1-0 iliyoupata katika mechi ya kwanza.**

Nyota huyo wa kimataifa wa England, Alli pia ataikosa mechi ya kwanza ya mtoano hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund.

Mechi ya marudiano, Ujerumani Machi 5, pamoja na ya 'dabi' Ligi Kuu England dhidi ya Chelsea, Februari 27, na ya Arsenal, Machi 2, pia zinaweza kuwa ni mapema kwa Alli.

Spurs ipo pointi tano nyuma kutoka timu inayoshika nafasi ya pili, Manchester City na nne mbele ya Chelsea kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Taarifa ya klabu hiyo ilisomeka: "Kufuatia vipimo na tathimini ya kitabibu, tunaweza kuthibitisha kuwa Dele Alli anasumbuliwa na majeraha ya misuli, aliyoyapata wakati wa mechi.

"Dele sasa atapata kipindi cha kuendelea kujiuguza na timu ya madaktari wetu, kwa matarajio ya kurejea mazoezini mapema Machi."

Alli baadaye 'alitwiti': " Nitafanya kila kitu kwa nguvu zangu kurejea mapema iwezekanavyo. Asante kwa meseji zenu wote."

## ZISIKUPITE

### AMCHELEWESHA RAMSEY

ARSENAL inaweza kumruhusu kiungo Aaron Ramsey, 28, kujiunga na Juventus mwezi huu kama itafanikiwa kukamilisha dili la kumsajili kiungo wa Barcelona, Mhispania Denis Suarez, 25, na Mcolombia James Rodriguez, 27, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Bayern Munich akitokea Real Madrid. ***(Independent)***

### MADRID YAMGEUKIA DYBALA

REAL Madrid imeanza kasi ya kumfukuzia mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala, 25, kwa pauni milioni 90. ***(Sun)***

### BAILLY AZUIWA ARSENAL

MANCHESTER United haitamruhusu beki Eric Bailly, 24, kutua Arsenal, ambayo ilikuwa tayari kumsajili jumla katika majira ya joto. ***(Mail)***

### BENITEZ ATISHIA KUSEBA

KOCHA Rafael Benitez anajiandaa kuondoka Newcastle United mwishoni mwa msimu, kinyume na hapo klabu hiyo isajili wachezaji wawili aliowahitaji mwanzoni mwa dirisha hili dogo. ***(Telegraph)***

### DE JONG ATESA VIGOGO

BARCELONA ipo katika nafasi nzuri zaidi ya kuzipiku Manchester City na Paris St-Germain katika mbio za kumsajili kiungo wa Ajax, Frenkie de Jong, 21. ***(Express)***

### SUAREZ BASI TENA ARSENAL

DILI la Arsenal kumpata Denis Suarez limevunjika kwa sababu miamba hiyo ya Emirates haitakubali kuihakikishia Barcelona kumsajili jumla Mhispania huyo. ***(Mail)***

### AZPILICUETA SHAKANI CHELSEA

NAFASI ya beki wa Chelsea, Cesar Azpilicueta ipo mashakani kufuatia kocha Maurizio Sarri kuwa tayari kumsajili beki wa kulia wa Napoli, Elseid Hysaj, 24. ***(Mirror)***

### UNITED, SPURS VITANI

MANCHESTER United inakabiliwa na ushindani kutoka Tottenham katika mchakato wa kumsajili winga wa PSV Eindhoven, Mholanzi Steven Bergwijn, 21. ***(Sun)***

### MONCHI KUULA ARSENAL

MKURUGENZI wa Soka wa Roma, Ramon Rodriguez Verdejo maarufu kama Monchi, ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kuwa mkurugenzi mpya wa ufundi wa soka wa Arsenal. ***(Independent)***

### AMTAJA AUBAMEYANG

KOCHA Sam Allardyce, amesema alitaka kumsajili straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, 29, kutoka Borussia Dortmund wakati akiinoa Everton. ***(Talksport)***

### PSG YAMTAKA GUEYE

PARIS St-Germain imetoa ofa kwa kiungo wa Everton, Msenegal, Idrissa Gueye, 29. ***(L'Equipe - in French)***

### BALOTELLI KUTUA MARSEILLE

STRAIKA Mtaliano Mario Balotelli, 28, amekubali kujiunga na Marseille akitokea kwa jamaa zao wa Ligue 1, Nice kwa mkataba wa miezi sita. ***(L'Equipe, via Mail)***

# KATWILA AWATUPIA LAWAMA MASTRAIKA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Shabani Katwila, amesema umakini mdogo wa washambuliaji wake ndio chanzo cha kufanya vibaya katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo imeingia katika duru la lala salama.

Mtibwa Sugar ambayo hivi karibuni ilitolewa na KCCA ya Uganda katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, imefungwa katika michezo mitatu mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema washambuliaji wake wanajitahidi kutengeneza nafasi, lakini umakini wao mdogo unawafanya washindwe kutumia vyema nafasi hizo na mwisho wa siku wanawaruhusu wapinzani kuondoka na pointi tatu.

**Katwila alisema bado analifanyia kazi tatizo hili na anaamini kikosi chake kitarejea kwenye makali yake, huku akiongeza kwamba timu zote zimejipanga kusaka ushindi.**

"Timu yangu inacheza vizuri, washambuliaji wangu wanatengeneza nafasi nyingi katika michezo yetu ila kinachotukwamisha ni kukosa umakini katika safu ya ushambuliaji, jambo ambalo limenifanya nikae chini na wachezaji wangu kutafuta mbinu mpya ya kutibu tatizo hili," alisema Katwila.

Aliongeza kuwa msimu huu mechi zote zimekuwa na ushindani na hakuna timu ndogo kwa sababu kila upande unaingia uwanjani ukiwa umejiimarisha kuhimili mikikimikiki.

Mtibwa Sugar ilianza kwa kufungwa mabao 2-0 na Tanzania Prisons halafu ikakubali kuchapwa na Mbeya City bao 1-0, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kufungwa 1-0 na Lipuli ya Iringa nyumbani kwenye Uwanja wa Manungu Complex.




Alex Peter (26), mkazi wa Kimara Temboni jijini Dar es Salaam, akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 31.1 na Mkurugenzi wa Uendeshaji SportPesa Tanzania, Luca Neghesti (kulia) juzi, kufuatia kuibuka mshindi wa bonasi ya Jackpot kutoka SportPesa baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

## Kilichomuua Oliver Mtukudzi

**HARARE,** Zimbabwe

MWANAMUZIKI mkongwe Afrika, Oliver Mtukudzi, amefariki dunia nchini Zimbabwe jana, wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Avenues, imethibitishwa.

Mkuu wa Masoko wa Lebo ya Gallo Records, Carol Marabe, ambayo mwanamuziki huyo raia wa Zimbabwe anaitumia alithibitisha kifo cha mwanamuziki huyo.

Hata hivyo, hakutaka kueleza zaidi ya hapo kwa madai kuwa wanaipa heshima familia ya mwanamuziki huyo na kwamba ndiyo itaeleza undani wa kifo chake, lakini habari kupitia mitandao mbalimbali jana zilieleza kuwa alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa kisukari.

Taarifa hizo zilizidi kueleza kuwa mwanamuziki huyo alikuwa hospitalini tangu Desemba mwaka jana.

Mtukudzi amefarikiwa akiwa na umri wa miaka 66, huku akiwa amesafiri pande mbalimbali za dunia, pamoja na kuzoa tuzo kibao, kitaifa na kimataifa. Ameshawahi kufanya ziara mara kwa mara nchini Tanzania na alimsaidia sana msanii Lady Jaydee kumshauri aanzishe bendi inayopiga muziki 'live' na si wa kutumia CD au kutengenezewa studio.

Alizaliwa mwaka 1952 na alianza rasmi muziki mwaka 1977.

Nchini Tanzania anakumbukwa mno na albamu yake ya mwaka 2001 ya 'Neria', ambayo pia iliingizwa kwenye filamu iliyojulikana kwa jina hilo, iliyokuwa ikipinga unyanyasaji wa kinamama wajane.



Lakini pia moja ya albamu zilizotia fora nchini ni 'Toddy', iliyokuwa na wimbo huo ambao ulitokea kupendwa sana. Baadhi albamu zake maarufu ni 'Bvuma, Shanda, Vhunze Moto, Dzoka Uyamwe', na nyingine nyingi.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 20 | 17 | 2 | 1 | 38 | 14 | 53 |
| 2. Azam | 19 | 13 | 5 | 1 | 27 | 8 | 44 |
| 3. Kinondoni MC | 22 | 8 | 10 | 4 | 29 | 16 | 34 |
| 4. Simba | 14 | 10 | 3 | 1 | 28 | 5 | 33 |
| 5. Lipuli | 22 | 8 | 9 | 5 | 17 | 13 | 33 |
| 6. Mbao | 23 | 8 | 10 | 5 | 16 | 19 | 33 |
| 7. Coastal Union | 21 | 6 | 10 | 5 | 20 | 21 | 28 |
| 8. Kagera Sugar | 21 | 6 | 10 | 5 | 19 | 20 | 28 |
| 9. Alliance | 23 | 7 | 7 | 9 | 19 | 27 | 28 |
| 10. Mtibwa Sugar | 18 | 8 | 2 | 8 | 19 | 15 | 26 |
| 11. Mbeya City | 21 | 7 | 5 | 9 | 24 | 26 | 26 |
| 12. JKT Tanzania | 22 | 5 | 10 | 7 | 10 | 15 | 25 |
| 13. Stand Utd | 22 | 7 | 4 | 11 | 21 | 29 | 25 |
| 14. Ruvu Shooting | 23 | 6 | 7 | 10 | 19 | 31 | 25 |
| 15. Mwadui | 23 | 6 | 6 | 11 | 24 | 22 | 24 |
| 16. Singida United | 21 | 6 | 6 | 9 | 15 | 20 | 24 |
| 17. Ndanda | 21 | 5 | 7 | 9 | 12 | 25 | 22 |
| 18. Biashara Utd | 22 | 4 | 8 | 10 | 13 | 21 | 20 |
| 19. African Lyon | 23 | 4 | 7 | 12 | 15 | 27 | 19 |
| 20. TZ Prisons | 21 | 2 | 11 | 9 | 12 | 21 | 17 |

# Sauti za Busara kukemea rushwa

**Na Elizabeth Zaya**

WASANII wanaotarajia kushiriki katika Tamasha la Sauti za Busara wameombwa kutumia jukwaa hilo kukemea vitendo vya rushwa ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na tatizo hilo.

Mkurugenzi wa Busara Promotions, Yusuf Mahmoud, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza maandalizi ya tamasha hilo ambalo litafanyika kuanzia Februari 7, mwaka huu huko Zanzibar yamekamilika.

Mahmoud alisema wasanii wa muziki kutoka katika nchi za Afrika ikiwamo Morocco, Nigeria, Zimbabwe, Algeria pamoja na nchi za Afrika Masharik, wanatarajia kutumbuiza katika tamasha hilo ambalo limefikia msimu wa 16.

"Kauli mbiu ya msimu wa tamasha hilo la busara mwaka huu inasema "Potezea rushwa sio dili" tukiwa na imani kwamba wasanii wanaweza kutumia sauti zao kukemea vitendo vya rushwa nchini, wakati wanasherehekea utajiri na mkusanyiko wa tamaduni mbalimbali za muziki wa Afrika," alisema Mahmoud.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Busara Promotions, Julia Bishop, alisema tamasha hilo limezidi kuwa bora kila mwaka, huku wastani wa watu wanaoshiriki kushuhudia wakiwa ni zaidi ya 20,000.

Naye Meneja wa tamasha hilo, Journey Ramadhani, alisema mwaka huu wanatarajia kuwa na majukwaa matatu ikiwamo ya Ngome Kongwe, Amphieter na ya wazi ambayo yatakuwa katika viwanja vya Forodhani kwa lengo la kutoa fursa ya wadau wengi zaidi kushuhudia tamasha hilo bure.

# Michezo

Alhamisi Januari 24, 2019

Nipashe




Kilichomuua Oliver Mtukudzi

HABARI UK. 31



Mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi, akipiga krosi, huku mchezaji wa AFC Leopards, Odenyi Jaffari, akijiandaa kuzuia, wakati wa mechi ya robo fainali ya Kombe la SportPesa iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana na Simba kushinda 2-1. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Simba yaitaka Everton

## ● ● ● Sasa kuivaa Bandari FC kesho, huku Mbao wakianza na Kariobangi Sharks kabla ya...

**Na Somoe Ng'itu**

SIMBA imeanza kuwafuta machozi mashabiki wake baada ya jana kutinga nusu fainali ya mashindano ya Kombe la SportPesa kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya AFC Leopards katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Bara, wamepata ushindi huo katika Uwanja wa Taifa, wakitoka kupigwa mabao 5-0 ugenini dhidi ya AS Vita ya DR Congo, kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Kwa matokeo hayo ya jana, sasa Simba itahitaji kushinda nusu fainali dhidi ya Bandari FC ya Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya pili ambayo itachezwa kesho, ili kuendelea kuweka matumaini ya kucheza dhidi ya Everton ya England.

Mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali itakuwa kati ya wababe wa Yanga, Kariobangi Sharks dhidi ya Mbao FC ya jijini Mwanza.

Mbao ilitinga hatua hiyo baada jana nayo kuwavua ubingwa, Gor Mahia ya Kenya kwa mikwaju ya penalti 4-3 kutokana na kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika ya 90 za kawaida.

Bingwa wa michuano hiyo hupata fursa ya kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya timu ya Everton ambayo nayo hudhaminiwa na Kampuni ya SportPesa kama ilivyo kwa Simba, Yanga na Singida United kwa hapa nchini.

Katika mechi ya jana, bao la kwanza la Simba lilifungwa dakika ya 13 na Mganda Emmanuel Okwi aliyemalizia krosi safi iliyopigwa na beki raia wa Ivory Coast, Zana Coulibaly.

Dakika ya 48 Mzambia, Clatous Chama, alifunga bao la pili akimalizia kazi nzuri iliyofanywa na Okwi aliyekuwa ndani ya 18.

Bao la AFC Leopards lilifungwa na Vicent Oburu dakika ya 61 baada ya kuwachekesha mabeki wa Simba na kipa wao, Manula akawa ameshapotea na kupiga shuti lililoingia moja kwa moja wavuni.

Simba ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa bao 1-0.

Hata hivyo, wageni AFC Leopards ndio walikuwa wa kwanza kufanya shambulizi kupitia kwa Mukangula Eugene, lakini akiwa jirani na lango la Simba alipiga pembeni wakati Simba ilikaribia kupata bao lingine dakika ya 19 kupitia kwa Okwi ambaye shuti lake lilidakwa na kipa Mkenya, Adira Jairus.

AFC walifanya shambulizi lingine kupitia kwa Wayela Tutawe, lakini beki wa Simba, Pascal Wawa, alimzuia vema na hivyo mpira kudakwa kirahisi na kipa, Manula.

Simba: Aishi Manula, Rashid Juma, Zana Coulibaly, Lamine Moro/Meddie Kagere (dk. 46), Pascal Wawa/Juuko Murshid (dk. 46), Jonas Mkude/James Kotei (dk. 46), Hassan Dilunga, Haruna Niyonzima, Hunlede Kissimbo, Emmanuel Okwi/Muzamil Yassin (dk. 66) na Clatous Chama.

# Sababu Fifa kumfungia Wambura maisha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), imemfungia maisha aliyekuwa Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Richard Wambura, kujihusisha na masuala yote yanayohusiska na mpira wa miguu ('football related activity'), imeelezwa.

Katika uamuzi wake uliotolewa juzi, Januari 22, mwaka huu na kutumwa TFF, Kamati ya Nidhamu ya Fifa chini ya Mwenyekiti wake, Anin Yeboah wa Ghana, imekazia hukumu ya Kamati ya Rufani ya Maadili ya TFF iliyotolewa Aprili 6, mwaka jana.



Hivyo kutokana na Kamati ya Nidhamu ya Fifa kukazia hukumu ya Kamati ya Rufani ya Maadili ya TFF, hatakiwi tena kujishughulisha na masuala ya mpira wa miguu duniani kote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, ilieleza kuwa TFF tayari imeshamkabidhi uamuzi huo Wambura na inawakumbusha wanafamilia wa mpira wa miguu kuzingatia maadili na nidhamu kwa kufuata taratibu zake kwa mujibu wa katiba za TFF, Caf na Fifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >